Nipashe
Jumatano Julai 17, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0581740
MWANGA WA JAMII
www.ippmedia.com
The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710
LIKE & FOLLOW US

**Samia** ataka wananchi kulipa kodi kuleta maendeleo

UKURASA 3

**Mbowe** alia madini tanzanite kutonufaisha Tanzania

UKURASA 8



**Trump** amchagua Vance mgombea mwenza

UKURASA 19




**KANE: NINA SONONEKO MOYONI**

UKURASA 22

# Waandishi wazuiwa kusikiliza ushahidi kesi aliyekuwa RC

UKURASA 2



Aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda (kushoto), akifuatana na wakili wake Constantine Mutalemwa jana kwenda katika chemba ya Hakimu Mfawidhi Mkuu wa Mahakama ya Mkoa wa Mwanza kwa ajili ya kusikiliza ushahidi wa shauri linalomkabili la ulawiti wa mwanafunzi wa moja ya vyuo mkoani Mwanza. **PICHA: VITUS AUDAX**

UKURASA WA 19

## KENYA MAANDAMANO YAFANYIKA TENA

MAANDAMANO ya amani yamerejea kote nchini Kenya kudai uwajibikaji na kuwakumbuka waliouawa katika wiki tatu za ....

## Wadau waibuka kauli ya Nape wadai inakiuka falsafa ya R4

UKURASA 5

# NIDA yatishia kusitisha matumizi NIN, Dar yaongoza kutochukua vitambulisho

UK. 7

**MICHEZO** SAKATA LA LAWI SIMBA, COASTAL MTIHANI KWA TFF UK.24

**MAONI,** UK.6

# Waandishi wazuiwa kusikiliza kesi ya aliyekuwa RC Simiyu

**Na Mwandishi Wetu**

KESI ya jinai inayomkabili aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda, jana imeanza kupokea na kusikiliza mashahidi katika Mahakama ya Hakimu Mfawidhi Mkoa wa Mwanza.

Hata hivyo, waandishi wa habari na wananchi hawakutakiwa kuingia mahakamani kusikiliza shauri hilo.

Kwa mujibu wa Sheria za Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 20 kifungu namba 186, shauri hilo lilitakiwa kuwa wazi.

Awali, shauri hilo lilitakiwa kusikilizwa katika ukumbi mkubwa wa Mahakama ya Hakimu Mfawidhi Mkoa, lakini bila taarifa yoyote, washtakiwa walipelekwa katika chemba ya hakimu huyo na kuanza kusikilizwa kuanzia majira ya saa tatu asubuhi.

Baada ya waandishi pamoja na wananchi waliofika mahakamani hapo kusikiliza shauri hilo kusubiri bila mafanikio, walidadisi kwa baadhi ya wahudumu wa mahakama hiyo ambaye aliwajibu kuwa tayari shauri hilo linaendelea ndani ya chemba.

Baada ya jibu hilo, waandishi walielekea katika mlango wa chemba hiyo, hata hivyo ilikuwa karibu na kipindi cha mapumziko cha dakika 35 ili warejee kusikiliza mashahidi.

Hakimu Mfawidhi Mkuu wa Mahakama hiyo, Erick Marley, alimtuma mmoja wa wasaidizi wake kuwaeleza waandishi kuwa hawatoruhusiwa kuingia katika chemba hiyo mpaka itakapotoka idhini ya mshtakiwa pamoja na shahidi kuruhusu kuwapo kwa waandishi pamoja na wasikilizaji wengine.

Kutokana na hali hiyo, waandishi wa habari walimfuata Msajili katika kituo hicho jumuishi ili kujua chanzo cha shauri hilo kuhamishwa ukumbi bila taarifa na wao kutoruhusiwa kuwapo wala wasikilizaji.

Msajili aliwasiliana na Hakimu Mfawidhi Mkuu, Erick Marley na kumtaka kuongea na waandishi kuhusu maswali yao na hakimu alikubali na kuwaita katika chemba yake na kuwaeleza kuwa hatua hiyo ni takwa la kisheria na haki ya mtoa ushahidi katika makosa ya namna hiyo.

Alipohojiwa kuhusu kifungu cha sheria kinachosimamia takwa hilo, Hakimu Marley alisema ni Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 20 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2022 Kifungu namba 186(3).

"Kufuatia takwa hilo mahakama itawahoji na kupata ridhaa yao baada ya mapumziko, na endapo wakikubali tutawaita waandishi na wale wanaohitaji kusikiliza shauri hili, lakini wasiporidhia hamtoruhusiwa."

Majira ya saa 11:23 washtakiwa pamoja na mashahidi walirejea katika chemba hiyo na waandishi waliendelea kukaa nje kwa muda bila kupata mrejesho hali iliyothibitisha walengwa kutokukubali kusikiliza shauri hilo.



**KIFUNGU NAMBA 186(a).**

Kwa Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai namba 20 iliyorejelewa mwaka 2022, kifungu hicho namba 186 (3) kinasema,

"Bila ya kujali masharti ya sheria nyingine yoyote, ushahidi wa watu wote katika kesi zote zinazohusu makosa ya kingono yatapokewa na mahakama kwa kamera (ikimaanisha bila kurekodiwa), ushahidi na mashahidi wanaohusika katika makosa ya kesi za namna hii haitachapishwa na au katika gazeti lolote au vyombo vingine vya habari.

Lakini kifungu hiki hakitapiga marufuku uchapishaji au usambazaji wa jambo lolote kama hilo kwa uaminifu mfululizo wa ripoti za kisheria au katika gazeti au majarida kwa nia njema inayokusudiwa kusambazwa miongoni mwa wanachama wataaluma wa sheria au matibabu."

Hakimu Mfawidhi Mkuu Marley aliahirisha shauri hilo na mashahidi hao walisikilizwa kwa zaidi ya saa tatu na nusu.

Hakimu Marley alisema kesi hiyo itaanza kusikilizwa mfululizo katika mahakama hiyo Agosti 13, 14 na 15, na kwamba Jamhuri ina mashahidi 15 na vielelezo 18, jana alisikilizwa mama wa binti anayedaiwa kuingiliwa kinyume na maumbile na binti mwenyewe.

# Tril.2.4/- hatarini kupotea kifisadi

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

TAASISI ya WAJIBU imechambua ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa mwaka 2022/23, ikibaini miamala mbalimbali yenye viashiria vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu.

Miamala hiyo inayofikia Sh. trilioni 2.41 imebainika kwenye ukusanyaji mapato, usimamizi wa matumizi ya fedha za serikali na ununuzi wa umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa, Serikali Kuu na Mashirika ya Umma.

Akiwasilisha ripoti ya uchambuzi huo jijini Dodoma jana wakati wa uzinduzi wa Ripoti za Uwabikaji 2022/23 za Taasisi ya WAJIBU, Meneja Programu za Utafiti na Miradi wa Taasisi hiyo, Moses Kimaro, alisema wamebaini kupungua kwa viashiria hivyo kwa miaka mitatu mfululizo.

Alifafanua kuwa mwaka 2020/21, miamala yenye viashiria hivyo ilikuwa na thamani ya Sh. trilioni 4.59, mwaka 2021/22 Sh. trilioni 3.8 na 2022/23 Sh. trilioni 2.41 katika Mamlaka za Serikali za Mitaa (halmashauri), Serikali Kuu na mashirika ya umma.

"Hata hivyo, uchambuzi wetu unaonesha kuongezeka kwa viashiria vya rushwa, udanganyifu na ubadhirifu katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kati ya mwaka 2021/22 (Sh. trilioni 297.86) na 2022/23 (Sh. bilioni 499.96)," Kimaro alisema.

Meneja huyo alitaja maeneo yenye viashiria hivyo yanajumuisha udhaifu katika usimamizi wa ununuzi wa umma (Sh. bilioni 440.49), mashirika ya umma kutumia fedha (Sh. bilioni 177.71) pasi na kufuata sheria, wizara kuingilia zabuni katika taasisi za umma (Sh. bilioni 10.4), bodi za zabuni kutoa zabuni kwa mzabuni asiye na sifa (Sh. bilioni 53.71) na shirika la umma kufanya machapisho bila mkataba (Sh. bilioni 1.71).

Vilevile, Kimaro alisema uchambuzi wao pia umegusa halmashauri 22 zilizofanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 28.87 nje ya mpango wa ununuzi wa mwaka husika na halmashauri 31 zilizonunua huduma zenye thamani ya Sh. bilioni 27.43 nje ya mfumo wa ununuzi.

Pia zimo halmashauri 16 zilizofanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 4.87 bila ushindani na halmashauri 14 zilizotia saini mikataba yenye thamani ya Sh. bilioni 9.95 bila kuhakikiwa na wanasheria wa halmashauri husika.

Kwa upande wa Serikali Kuu, Kimaro alisema taasisi 10 zilifanya ununuzi wenye thamani ya Sh. bilioni 2.11 bila kuidhinishwa na bodi za zabuni, taasisi 16 zilinunua bidhaa zenye thamani ya Sh. bilioni 149.56 nje ya mfumo wa kielektroniki huku nne zikinunua bidhaa za Sh. bilioni 2.16 bila mikataba.

**NINI KIFANYIKE?**

Kimaro alishauri serikali iendelee kuchukua hatua za kinidhamu na kisheria dhidi ya watumishi wote waliohusika na matumizi mabaya ya rasilimali za umma ikiwamo kuvitaka vyombo vya uchunguzi (Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa - TAKUKURU), Ofisi ya Mkurugenzi wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai (DCI) na Ofisi ya Taifa ya Mashtaka kuwafikisha mahakamani wahusika hao.

Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya WAJIBU, Ludovick Utouh, CAG mstaafu, alishauri serikali kupitia Bunge, itunge Sheria ya Kuzuia Wizi wa Fedha za Umma (Anti-Fraud Act) ambayo anaamini itarahisisha kuwawajibisha wote watakaohusika na vitendo vya rushwa, ubadhirifu na udanganyifu dhidi ya fedha za umma.

Pia alishauri Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) iandae mkutano kati ya CAG na maofisa masuuli ili kujadili kwa pamoja sababu za maofisa hao kutotekeleza kikamilifu hoja za ukaguzi zinazotolewa kwao, takwimu zikionesha utekelezaji wa mapendekezo ya CAG uko chini ya asilimia 40.

Ni hoja iliyoungwa mkono na Edward Simon kutoka Asasi ya Kioo ya mkoani Kigoma, akiamini hatua hiyo itasaidia kujibu swali, "shida ni dawa haina kiwango, mgonjwa ana usugu wa dawa au mgonjwa hataki kumeza dawa?"

Mkurugenzi wa Kujenga Uwezo katika Ununuzi wa Umma wa Mamlaka ya Usimamizi wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Awadhi Suluo, aliyekuwa mgeni rasmi katika uzinduzi wa ripoti hizo, alisema:

"Kama raia wa Tanzania, tuzingatie wajibu wetu uliotajwa katika Ibara ya 8 na 27 za Katiba ya nchi yetu. Hizi ripoti zimerahisishwa ili hata mwananchi mwenye kiwango cha chini ya elimu aelewe. Ninapongeza Taasisi ya WAJIBU kwa kuandaa ripoti hizi kwa miaka minane mfululizo."

## HABARI KITAIFA

# Samia ataka wananchi walipe kodi kuleta maendeleo

**Na Jenifer Gilla**

RAIS Samia Suluhu Hassan, amewakumbusha Watanzania kulipa kodi ili isaidie kutekeleza miradi ya maendeleo ikiwamo ujenzi wa barabara.

Aidha, ameonya madereva wanaoendesha mwendokasi kwenye barabara mpya, kwa kuwa wanachangia ongezeko la ajali na kuitia hasara serikali kugharamia matibabu ya majeruhi.

Rais Samia aliyasema hayo jana katika ziara ya siku tatu mkoani Rukwa ambako alizindua jengo la utawala Halmasauri ya Wilaya ya Kalambo, barabara ya Sumbawanga-Matai -Kasanga yenye urefu wa Kilometa 107.14 wilayani humo.

Pia, alizindua maghala ya kuhifadhia nafaka, kuweka jiwe la msingi Chuo cha Ufundi VETA, Uwanja wa Ndege wa Sumbawanga katika halmashauri ya Sumbawanga na Chuo cha Ualimu Sumbawanga.

Alisema ili nchi itekeleze miradi ya maendeleo wananchi hawana budi kulipa kodi zinazowekwa na serikali haijalishi ni ndogo au kubwa ili mradi iwe halali.

"Kwa hiyo pale tunapopenyeza vitozo vidogo vidogo vile vya halali lipeni ili tukusanye tuweze kuwarudishia ujenge mabarabara, tujenge hayo madaraja, mashule na mambo mengine, kwa sababu hakuna serikali inayoendeshwa kwa pesa nyingine zozote isipokuwa pesa za kodi za wananchi wake," alisema Rais.

Alisema kuna baadhi ya madereva wanaendesha kwa mwendo kasi pale wanapita kwenye barabara mpya, jambo linalochangia ongezeko la ajali na kuitia serikali hasara ya kugharamia matibabu, kwa kuilazimu kujenga vituo vya matibabu ya dharura.

Rais Samia alisema pia kuna madereva wanaoegesha magari pembezoni mwa barabara kwa sababu mbalimbali, ikiwamo kufanya matengenezo na baadhi yao yanamwaga dizeli kwenye barabara na kusababisha kuharibika.

Aliwaonya wananchi kuacha tabia ya kuchimba na kulima pembezoni mwa barabara kutokana na kusababisha mmomonyoko wa udongo na kuharibu miundombinu hiyo.

Alisema inasikitisha ukipita kwenye baadhi ya barabara unaona pembeni imeliwa (kuchibwa) jambo linalosababisha kudumu kwa muda mfupi na kuitia serikali hasara na kuwaagiza wasimamizi wa barabara wa wilaya zinakuwa salama.

"Ukijenga kilometa moja tu ya barabara ni sawa na kujenga vituo vitatu vya afya vya kata pamoja na kuweka vifaa tiba ndani yake, kwa hiyo niwaombe tuitunze barabara yetu," alisema.

Alisema serikali inajipanga kujenga barabara ya mchepuko kuelekea eneo la Laela, ili kuungana na barabara hiyo kuelekea katika Bandari ya Kasanga hali itakayokuza biashara na nchi jirani.

Kadhalika, alisema jengo la Halmashauri ya Kalambo litarahisisha uratibu na utoaji huduma muhimu kwa wananchi wa eneo hilo kwa kuweka pamoja mtendaji mkuu, madiwani na wakuu wa idara zote na kuwasisitiza viongozi hao kufanya kazi kwa pamoja.

Kwa mujibu wa Rais Samia, serikali inaendelea na ujenzi ya hospitali ya wilaya na mpaka sasa imetumia Sh. bilioni 1.64 na ujenzi unaendelea huku baadhi ya huduma kama vile uzazi na mtoto zimeanza kutolewa.

Akizindua vihenge na maghala ya kuhifadhia nafaka, katika Kijiji cha Kanondo, Rais Samia alisema lengo ni kuboresha uhifadhi na kuwaondolea wakulima mzigo wa dhuluma uliokuwa unafanywa na mawakala hapo awali na kukuza uzalishaji.

Aidha, aliwaomba wakulima hao kuacha tabia ya kuuza vyakula hivyo kwa watu wasiokuwa na vibali ambao pia ni walanguzi na matokeo yake kinapelekwa nje ya nchi kinyemela na serikali inakosa mapato.

Aliwataka kuuza bidhaa hiyo kwa Wakala wa Taifa wa Hifadhi ya Chakula (NFRA) kwa bei nafuu ambao ndio huuza nje ya nchi kwa bei iliyopangwa na faida inayopatikana husaidia wakulima kupata ruzuku kwenye pembejeo za kilimo.

Rais aliwaomba wananchi wa Mtaa wa Kashai, wakitumie chuo cha VETA kilichojengwa katika eneo hilo vizuri kwa kuwapeleka watoto wao ili kuzalisha vijana wenye ujuzi watakaotumia rasilimali za nchi kujiletea maendeleo kwa kujiajili au kuajiriwa.

Akizungumza na wananchi wa Mkoa wa Rukwa, aliwaomba kuelekea uchaguzi wa serikali za mitaa Oktoba, mwaka huu, wakichague Chama Cha Mapinduzi (CCM) ili kuipa nguvu serikali kutekeleza miradi ya maendeleo.

"Kwa hiyo niwaombe sana ndugu zangu, tukafanye vizuri kwenye chaguzi hizo zinazokuja ili kazi yetu ya maendeleo iendelee," alisema.

Akizungumzia ujenzi wa barabara hiyo, Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Barabara Tanzania (TANROAD), Mohamed Besta alisema umegharibu Sh. bilioni 150.5 ikijumuisha ujenzi, ushauri na fidia kwa wananchi waliopisha eneo.

Alisema Uwanja wa Ndege wa Rukwa unafadhiliwa na Benki ya Uwekezaji ya Ulaya na utajengwa kwa kiwango cha lami yenye urefu wa 11.75 na kupokea ndege zenye uwezo wa kubeba abiria 50 hadi 60.

Mwanafunzi wa ushonaji VETA, Anasatazia Godfrey, alisema chuo hicho kimemrahisishia upatikaji wa elimu na atakapomaliza elimu yake atakwenda kujiajiri, alimshukuru Rais kwa kupigania ujenzi wa chuo hicho.


**Jinsi Ya Kununua Magazeti Ya Nipashe na The Guardian katika tovuti ya www.ippmedia.com au epaper.ippmedia.com**

**Kupitia tovuti ya epaper.ippmedia.com:**

1. Utafungua tovuti ya **epaper.ippmedia.com** utachagua toleo unalotaka kununua aidha Nipashe au The Guardian kwa kuclick Read
2. Itakuletea ukurasa mwingine unaotakiwa kujaza taarifa zako na kifurushi unachotaka kujiunga. Kisha unabonyeza **"subscribe"**
3. Itakupeleka katika ukurasa wa malipo ambapo unaweza kulipa kwa **kadi ya benki** malipo kwa **mtandao wa simu** unaoutumia baada ya kujaza kwa usahihi taarifa zako na anuani
4. Kwa **namba ya simu** unachagua mtandao wa simu unatumia ambapo utaandika namba yako na kutick box la kukubali terms and conditions. Itakuletea maelekezo kwenye simu yako namna ya kulipa ambapo utaweka namba ya siri na kuruhusu muamala. Malipo yakikamilika, utapokea email na message kuwa pesa imepokelewa hivyo utaingia kwa account yako na kuanza kusoma yale matoleo umeyalipia
5. **Kwa benki** unaweka taarifa za kadi yako ndio uruhusu muamala ukatwe katika account yako baada ya kukubali terms and conditions. Ndipo utaingia katika account yako na kusoma toleo ulilolilipia

**Na kwa tovuti ya www.ippmedia.com**

6. Unafungua website yako ya **www.ippmedia.com** upande wa kulia utaona **"E-Paper"** utabonyea na kuafuatisha hatua zote 1-5



For more Information Contact 0677 020 701 | Subscription: 0625 174 714 | Email: customerrelations@guardian.co.tz

Nipashe The Guardian

# Madereva wawili wa malori wateketea ajalini

**Na Said Hamdani,** LINDI

MADEREVA wawili wamefariki dunia papo hapo kwa kuteketea kwa moto na abiria mmoja kujeruhiwa baada ya malori waliyokuwa wakiendesha kugongano uso kwa uso na kulipuka moto.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP), John Imori, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo katika Kijiji cha Mkwaya, barabara kuu Lindi Mtwara Julai 14, mwaka huu, majira ya saa 8:50 mchana.

Aliwataja waliofariki katika ajali hiyo kuwa ni Daudi Mdota (44) wa Kampuni ya Saruji ya Dangote Mkoa wa Mtwara na Jafari Abdull Omari (39) wa Kampuni ya Specialized Haulers Ltd, gari lake lililokuwa limebeba makaa ya mawe.

Aliyekuwa abiria Saidi Mussa (22) katika gari la Specialized Haulers Ltd, amelazwa Hospitali ya Sokoine mjini Lindi, huku hali yake ikiwa mbaya kutokana na malori hayo kuungua moto.

Alisema Daudi alikuwa anaendesha lori lenye namba za usajili T 234 DZT kutoka Dar es Salaam kwenda Mtwara na Jafari Omari akiendesha lori lenye namba za usajili T 132 DUJ mali ya kampuni ya Specialized Ltd kutoka Mtwara kwenda jijini Dar es Salaam.

Kamanda Imori alisema chanzo cha ajali ni uzembe uliofanywa na dereva wa Kampuni Dangote kutoka upande wa kushoto kwenda kulia na kukutana na lori lingine uso kwa uso na kulipuka moto.

"Baada ya haya magari kugongana uso kwa uso yaliwaka moto na kuteketea yote mawili papo hapo," alisema Kamanda Imori.

Aliwataka madereva kuwa makini wanapokuwa wakiendesha vyombo vya moto ili kuepusha ajali kwa wananchi wengine wakiwamo wanaotembea kwa miguu.

Mganga Mfawidhi Hospitali ya Sokoine, Dk. Alexander Makalla, alithibitisha kupokea majeruhi mmoja ambaye hali yake sio nzuri kutokana na sehemu kubwa ya mwili wake kuungua moto.

Mmoja wa abiria aliyekuwa anasafiri na lori la Dangote kutoka Mnazi Mmoja Lindi kwenda Mtwara, ambaye hakupenda jina lake litajwe alisema anamshukuru Mungu baada ya kushushwa njiani na dereva wa lori hilo ambaye alimshauri asimame ili amwangalie mwendesha pikipiki aliyekuwa amemsukuma na kuanguka.

"Nikiwa Mnazi Mmoja nilipanda gari la Dangote kwenda Mtwara, tulipofika Kijiji cha Mkwaya, dereva akamsukuma mwendesha pikipiki na kuanguka chini bila kusimama, nilipomshauri asimame ili akamwangalie akaamua kunishusha," alisema abiria huyo.

Alisema baada ya lori hilo kutembea umbali mfupi likagongana na lori la kubeba makaa ya mawe na kulipuka moto na kuteketea.

# Mwalimu akutwa amejinyonga hadi kufa

**Na Cynthia Mwilolezi,** SIMANJIRO

MWALIMU wa Shule ya Awali na Msingi New Vision iliyopo katika Mamlaka ya Mji Mdogo wa Mirerani, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara, anadaiwa kujinyonga hadi kufa kwa kutumia kamba ya manila.

Kamanda wa Polisi wa Mkoa wa Manyara, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP), George Katabazi, akizungumza na waandishi wa habari jana alimtaja mwalimu huyo kuwa ni John Msinga (34), mkazi wa kitongoji cha Songambele.

Alisema Msinga alifariki dunia kwa kujinyonga akiwa ndani ya ghala la kuhifadhia chakula cha shule hiyo.

"Mwalimu huyo alijinyonga kwenye stoo ya kuhifadhi mahindi ya shule hiyo kwa kutumia kamba aina ya manila na akafariki dunia papo hapo," alisema Kamanda Katabazi.

Alisema tukio hilo lilitokea Julai 14, mwaka huu, saa 10:00 jioni, baada ya mwangalizi wa watoto wa shule hiyo, Paulo Essau, kukuta mwili wake ukiwa umening'inia kwenye ghala hilo.

Alisema hadi sasa hawajabaini chanzo cha tukio hilo na polisi wanaendelea na uchunguzi, hakuna mtu wanayemshikilia kutokana na kifo hicho.

Mwili wa marehemu umehifadhiwa kwenye chumba cha maiti cha Kituo cha Afya Mirerani.


Alipoulizwa kuhusu tukio hilo, Mkurugenzi wa shule hiyo, Prisca Msuya, alisema hafahamu chanzo cha mwalimu huyo kujinyonga.

Alisema mwalimu huyo alikuwa amekwenda nyumbani kwao hivi karibuni na kurudi baada ya wiki moja, lakini alikuwa mkimya mno.

"Alikuwa mpweke mno kila wakati ni mkimya na akiulizwa hajibu kitu chochote kile, mara nyingi akawa amejitenga peke yake bila kuwa na mtu," alisema.

Alisema ingekuwa vyema kama angezungumza chochote kinachomsibu.

Kwa mujibu wa Mkurugenzi huyo, wanawasubiria ndugu wa marehemu, ambao wataamua taratibu za maziko.



*Magistrates Court (Approved Forms for the Primary Court)*

*GN. NO. 943 (Contd.)*

*FOMU MADAI - 3*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI

Kituo cha MAGOMENI Mkoa DAR ES SALAAM

Shauri la Madai/~~Ndoa~~ Na 108/20 24

Jina la mdai HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINON

Jina la Mdaiwa FADHIL Y. KARIM, REYTON R. PAUL, KONDO S. MOHAMED

KUITWA SHAURINI MDAIWA

(*Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo*)

Kwa FADHIL Y. KARIM, REYTON R. PAUL, KONDO S. MOHAMED

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba (*Eleza hapa habari za Madai*) FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 22 Mwezi 7 Mwaka 2024 Saa 3:00 asubuhi/~~Mchana~~ kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.


ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20 Mwezi 6 Mwaka 2024

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO MAGOMENI - KINONDONI

PRIMARY COURT MAGOMENI DAR ES SALAAM TANZANIA



*Magistrates Court (Approved Forms for the Primary Court)*

*GN. NO. 943 (Contd.)*

*FOMU MADAI - 3*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

THE JUDICIARY OF TANZANIA MAHAKAMA YA TANZANIA

MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI

Kituo cha MAGOMENI Mkoa DAR ES SALAAM

Shauri la Madai/~~Ndoa~~ Na 109/20 24

Jina la mdai HALMASHAURI YA MANISPAA YA KINON

Jina la Mdaiwa LAWRENCE KURWA SAMWEL, BARAKA ANASE SHAO, LAWRENCE DOTO SAMWEL

KUITWA SHAURINI MDAIWA

(*Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo*)

Kwa LAWRENCE KURWA SAMWEL, BARAKA ANASE SHAO, LAWRENCE DOTO SAMWEL

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba (*Eleza hapa habari za Madai*) FIKA MAHAKAMANI BILA KUKOSA

Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 22 Mwezi 7 Mwaka 2024 Saa 3:00 asubuhi/~~Mchana~~ kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20 Mwezi 6 Mwaka 2024

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO MAGOMENI - KINONDONI

PRIMARY COURT MAGOMENI DAR ES SALAAM TANZANIA

38

HABARI KITAIFA

# Msigwa: Samia ana njia anayowapeleka Watanzania

**Na Romana Mallya**

MCHUNGAJI Peter Msigwa aliyehamia Chama Cha Mapinduzi (CCM) akitokea Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), amesema Rais Samia Suluhu Hassan ana njia anayowapeleka Watanzania.

Alisema hayo jana katika mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya Pangas, Kata ya Wazo, Jimbo la Kawe, Wilaya ya Kinondoni,mkoani Dar es Salaam, wakati wa ziara ya Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amos Makalla anayoifanya mkoani humo.

Msigwa ambaye amekuwa mbunge kupitia CHADEMA kwa miaka 10, Mwenyekiti wa Kanda ya Nyasa (yenye mikoa mitano) na mjumbe wa Kamati Kuu katika chama alichotoka, alisema Rais Samia ana mahali anakowapeleka.

"Ukienda kwenye huduma za afya, hata Iringa kuna mambo makubwa yamefanyika, vituo vya afya na vifaa tiba, machinga maeneo mengi licha ya changamoto, lakini kazi kubwa imefanyika," alisema Msigwa ambaye hivi karibuni alipokewa na Mwenyekiti wa Taifa CCM, Rais Samia.

Alisema hata alipokuwa bungeni aliwahi kutoa shilingi kuwatetea machinga na ameona Rais Samia anafanya kazi ikiwamo katika miundombinu.

"Kuna mwelekeo, mama anafanya kazi. Katika sekta ya elimu anafanya kazi. Nchi ilikuwa imefungwa mama kaifungua. Tunaona wawekezaji wanakuja.

"Ukimuuliza 'Nkururinza' maono yako ni yapi? Utasikia kunja ngumi, watu wamekunja ngumi mpaka wameota vibiongo, wakiinua ngumi yeye nyumba zinainuka, wakiinua ngumi yeye magari yanaongezeka.

"Nimekuwa mwenyekiti wa kanda utajijua mwenyewe nilikuwa na majimbo 31 utasafiri mwenyewe kujenga chama, usiposafiri anasema hufanyi kazi, yeye anaruka na chopa (helikopa)," alidai Msigwa.

Alisema wajibu wake sasa ni kujenga CCM ili kishinde katika uchaguzi za Serikali za Mitaa mwaka huu na Uchaguzi Mkuu mwakani.

Alisema amekuwa CHADEMA zaidi ya miaka 20 na aliingia huko kutokana na kuvutiwa na sera nzuri, lakini baada ya kukaa akaanza kuwafahamu ni tofauti na matendo yao.

Alisema walikuwa ni watu wa kudandia hoja na kutoa maneno bila majibu.

Alidai kuwa CHADEMA haitendi haki uamuzi unafanywa na mtu mmoja baada ya kufanya kikao nyumbani kwake na akienda katika kikao cha chama anataka ndio ufuatwe.

"Moyo umenisuta wa kuikemea CCM kwamba haitendi haki, sipati huo ujasiri nimefanya uamuzi mgumu na sahihi kuhamia CCM," alisema.

Msigwa aliutaka upinzani hasa vijana wenye shahada usome ramani kwa kuwa huko kuna matumaini feki.

Makalla akihutubia katika mkutano huo alisema Msigwa amewakosha hivyo watamtumia kuupiga upinzani wakati yeye akielezea mzuri yaliyofanywa na serikali.

"Jiulize mtu kama Msigwa kajitoa miaka 10 CHADEMA kwa hali na mali na ni mchungaji hasemi uongo alafu ameamua kutoka, wewe nani undelete kubaki, leo tunapokea hapa mpaka walinzi waliokuwa wanawalinda, hongera Msigwa umenirahisishia kazi yangu.

"Nikuahidi kazi ndo imeanza tukimaliza ziara ya Mkoa wa Dar es Salaam tutaanza ya Katibu Mkuu CCM," alisema.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Albert Chalamila, alisema kitendo cha wafanyabiashara Soko Kuu la Kariakoo kwenda ofisi ndogo za CCM, Lumumba, aliona ni ushari kwa kuwa waliruka ofisi zote za chini ikiwamo yake kwenda kumshtaki.

"Cheo ninakitaka na mimi ni mwanachama nisiyetiliwa shaka. Kwenda moja kwa moja Lumumba ni kuonesha kama ofisi ya CCM Wilaya haipo, ofisi ya Mkuu wa Wilaya haipo na ofisi ya Mkuu wa Mkoa haipo. Ninaomba niwaambie mimi nipo.

"Juzi tumeona vijana wa Soko la Simu 2000. Tuache usanii na unafiki tuilinde amani yetu, tusifurahie mabomu, tunaona nchi za wenzetu," alisema.

Mbunge wa Kawe, Josephat Gwajima, alisema changamoto kubwa iliyobaki katika jimbo hilo ni barabara ambazo kutokana na mvua, mito imepanuka na kuathiri makazi ya watu na baadhi ya nyumba kusombwa.

Alisema katika mwaka huu wa fedha, serikali imetoa Sh. bilioni moja kudhibiti changamoto hiyo.

Gwajima alisema waliahidi kutoa gari la kubeba wagonjwa na jana wamekabidhi ya pili ili kusaidia kutoa huduma Kituo cha Afya Nyakasangwe, Kilichopo Mtaa wa Nyakasangwe, Kata ya Wazo na maeneo mengine.




Kiongozi wa Timu ya 27 ya Madaktari wa China, Zhang Jungiao (kushoto) na Daktari Bingwa wa Upasuaji wa Moyo, Liu Yimin (kulia), wakiongea na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam kuhusu mafanikio yaliyopatikana tangu awamu ya kwanza ya madaktari kutoka China ilipowasili nchini kutoa huduma mwaka 1964 hadi sasa. **PICHA: FRANK MONYO**

# Wadau waibuka kauli ya Nape

## •Makala asema si ya CCM

**Halfani Chusi na Romana Mallya**

KAULI ya Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye imeibua wadau wa siasa nchini na kusema si njema kwa ustawi wa demokrasia.

Ni baada ya Waziri Nape kusikika akiwa katika Jimbo la Bukoba Mjini akisema matokeo ya kura sio lazima yawe kwenye boksi, inategemea nani anahesabu na nani anamtangaza mshindi.

Pia alisikika akisema kuna uchaguzi wa halali, nusu halali na haramu, jambo lilizoua taharuki katika mitandao ya kijamii na wadau wa siasa nchini.

Akipinga kauli hiyo, Mkurugenzi wa Mawasilinao, Uenezi na Mambo ya Nje wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), John Mrema, alisema ni kauli ya hatari kwa mustakabali wa demokrasia ya nchi ikizingatiwa imesemwa na mteule wa Rais.

Alisema kauli hiyo inamchafua Rais Samia moja kwa moja na ni ya kukemewa na kila Mtanzania kwa kuwa inapingana na falsafa yake ya R4.

"Lakini huyu Nape hajanishangaza kwa sababu yeye hajawahi kushinda uchaguzi kwa halali, kwa hiyo hajui nini maana ya uchaguzi.

"Mwaka 2020 kule Mtama, mgombea wetu Suleimani Mathew, alikamatwa siku ya kurejesha fomu akiwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Halmashauri ikapelekea akashindwa kuirejesha."

Alisema kama Rais Samia haungi mkono kauli hiyo, amchukulie hatua mara moja vinginevyo wataamini kwamba ndicho wanachojadili kwenye Baraza la Mawaziri kwa sababu Nape pia ni mjumbe.

Naibu Mwenezi wa Chama cha ACT-Wazalendo, Shangwe Ayo, alisema chama chao kinalaani kauli hiyo na kwamba wanapaswa kujua vyama vya upinzani vimejipanga na asifikirie uchaguzi huu utakuwa kama wa mwaka 2020.

"Tunamshangaa sana Rais Samia amekuja na falsafa ya R4 lakini watu wake wa chini wanashindwa kuzifuata inatupa wasiwasi kama hizo falsafa ni hadaa za kutuchelewesha na kufanya tumpe imani yetu ambayo tayari ameshaitumia vibaya, asidhani kwamba uchaguzi ujao utafanana na uliopita tupo tayari kulinda na kupiga kura kwa nguvu zote.

**MAKALLA ATOA KAULI YA CCM**

Akizungumza katika mkutano wa hadhara uliofanyika viwanja vya Pangas, Kata ya Wazo, Jimbo la Kawe, Wilaya ya Kinondoni, mkoani Dar es Salaam, wakati wa ziara yake, Katibu wa NEC, Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amos Makalla alijibu kauli iliyotolewa na Nape si ya CCM.

Alisema amesikia mitandaoni kuna kiongozi anasema eti ushindi wa uchaguzi hautokani na kura za kwenye boksi.

"Mimi ninataka niwaambie hiyo kauli isitazamwe kuwa inatokana na CCM," alisema Makalla.

Alisema kauli hiyo sio msimamo wa chama hicho na kwamba, CCM kinaheshimu demokrasia na kuamini vyama vyote vitashindwa na CCM kitashinda kwa haki na kitaheshimu uamuzi wowote aliyeshinda ndiye atakayetangazwa.

Alisema CCM kinaamini kuhusu tume huru na utawala bora.

Nnauye ambaye amewahi kuwa Katibu wa Halmashauri Kuu ya CCM, Itikadi na Uenezi, alitoa kauli hiyo juzi usiku alipotembelea soko la Kashai, mkoani Kagera na kuzungumza na wananchi.

"Unajua nyie sikilizeni, matokeo ya kura sio lazima yawe ya kwenye boksi, inategemea nani anahesabu na kutangaza.

"Na kuna mbinu nyingi kuna halali, nusu halali na kuna haramu na zote zinaweza kutumika ilimradi tu mkishamaliza unamwambia Mwenyezi Mungu nisamehe pale nilipokosea," alisema.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Mliokuwa mkilalamika kukosa vitambulisho NIDA kachukueni

**WAKATI** Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), ilipokuwa ikatangaza watu kujiandikisha kwa ajili ya kupata vitambulisho hivyo, wengi walikuwa wakisuasua na kuona ni suala lisilo na umuhimu.

Pamoja na wananchi kupewa elimu ya umuhimu wa kuwa na vitambulisho hivyo, mwamko haukuwa mkubwa sana.

Vitambulisho vya NIDA vina kazi kubwa na ni muhimu kuwa navyo kutokana na kuhitajika kila mwananchi anapohitaji huduma.

Kwa mfano mtu anapokwenda benki kufungua akaunti ataulizwa kitambulisho hicho, anapotaka kupata hati ya kiwanja, anapotaka huduma ya maji au umeme, atatakiwa kutoa kitambulisho cha NIDA. Na wengi wanakwama kupata huduma hizo kwa kukosa kitambulisho hicho.

Baada ya wananchi kupata adha hizo na kuamua kwenda kujiandikisha kwa ajili ya kupata vitambulisho hivyo, Mamlaka ya Vitambulisho ilitoa namba za utambulisho ambazo zilisaidia watu kupata huduma hizo muhimu.

Sababu za kutoa namba kwanza ni kutokana na Mamlaka kusubiri vitambulisho vichapishwe ili watu wapate kadi.

Sasa kadi ziko tayari, lakini wananchi waliokuwa wanalalamika kucheleweshwa kupatikana kwa kadi hizo, hawajaenda kuzichukua.

Kutokana na hali hiyo Mamlaka hiyo imetoa angalizo kwamba itafika hatua watasimamisha utaratibu wa watu kupatiwa huduma kwa kutumia namba za utambulisho (NIN), endapo wananchi wataendelea kupuuza kwenda kuchukua vitambulisho vyao ambavyo tayari vimeshatoka.

Mamlaka hiyo imebaini kuwapo mrundikano mkubwa wa vitambulisho hivyo katika ofisi za serikali za mitaa, kata, vitongoji, vijiji, wilaya na mikoa, kutokana na wahusika kutokwenda kuvichukua, huku Mkoa wa Dar es Salaam ukitajwa kuongoza kutokana na wengi kutegemea kutumia namba walizopatiwa awali.

Oktoba 2023, Mamlaka ilianza uzalishaji mkubwa wa Vitambulisho vya Taifa na kuvisambaza kwa wingi katika maeneo mbalimbali katika mikoa, wilaya na vijiji.

Hiyo ilikuwa ni kukidhi mahitaji ya wananchi ambao walikuwa wakilalamika kuwa hawana vitambulisho na wanakosa huduma.

Baada ya kusikia malalamiko ya wananchi, Mamlaka ilipata imani kwamba endapo watazalisha na kusambaza, ndani ya muda mfupi watajitokeza kwa wingi na kuchukua, akieleza kuwa kwa sasa hali ni tofauti na walivyotarajia kwakuwa kasi ya wananchi sio kubwa hasa katika maeneo ya mijini.

Mkoa wa Dar es Salaam umebainika kuwa uko chini kwa takwimu za kuchukua vitambulisho kuliko mingine, licha ya kuongoza kwa malalamiko ya watu kuonyesha uhitaji.

Alisema tatizo hilo linachangiwa na watu kuendelea kupatiwa huduma kwa kutumia namba za utambulisho wa taifa na kwamba hiyo inasababisha wananchi kutokuona haja ya kwenda kuchukua kitambulisho hata kama anajua kuwa kimetoka.


Tatizo lingine ni watu kuhama katika maeneo waliyojiandikishia ikiwamo watumishi wa umma na wanafunzi wa elimu ya juu ambao wameshamaliza masomo wameajiriwa katika maeneo mengine, huku nyuma vitambulisho vimetoka inakuwa shida kuja kuchukua.

Utaratibu wa kuchukuliwa kitambulisho inahitaji kuzingatia mhusika kutakiwa kuandika barua ya kumtambulisha atakayekwenda kumchukulia na ataweka sahihi yake, anaenda kuchukua naye ataandika nyingine kwamba ataenda kumchukulia ndugu yake, ataandika majina yake, namba ya simu na kivuli cha namba ya utaifa.

Wananchi waache kisingizio cha kutokuchukua kitambulisho kutokana na umbali kwa kuwa mamlaka imeweka utaratibu mzuri wa kuchukuliana.

Lengo la serikali la kuweka utaratibu wa kila mwananchi kuwa na kitambulisho cha utaifa ni pamoja na kuimarisha usalama na kuwa na taarifa muhimu za kila Mtanzania.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Sabato Kasika

# Hongera CCM kuwabana wasiokubalika lakini...

**UCHAGUZI** wa viongozi wa serikali za mitaa unatarajiwa kufanyika Oktoba mwaka huu, ni wakati ambao Watanzania watachagua watakaowaongoza kwenye mitaa, vijiji na vitongoji kwa miaka mitano ijayo.

Wakati maandalizi ya uchaguzi yakiendelea, CCM inasema msimamo wake kuhusu uchaguzi huo, safari hii, haitaweka wagombea ambao si chaguo la wananchi.

Sababu za kuja na msimamo huo, zinaelezwa na Katibu wa NEC, Siasa, Itikadi, Uenezi na Mafunzo CCM Taifa, Amos Makalla, kuwa ni kutokana na fundisho chama kilicholipata.

Makalla anasema kimebaini kuwa mgombea anayekataliwa na kisha chama kikampitisha, anakuwa sio matakwa ya wapigakura na kwamba anaweza kusababisha chama kushindwa katika uchaguzi.

Hatua hiyo ya CCM kuweka pembeni wagombea wasiokubalika inagusa kaulimbiu ya uchaguzi wa serikali za mitaa mwaka 2019 iliyokuwa inasema; "viongozi bora wa serikali za mitaa ni chachu ya maendeleo."

Makala anasema: "Tumeshaelezana Halmashauri Kuu za wilaya msibebe wagombea ambao siku mnamweka tu watu wanaanza kuguna. Tunaahidi kuweka wagombea bora, wanaokubalika na kuwatumikia wananchi."

Kwa kauli hiyo, ni wazi kwamba wagombea ambao hawana uwezo wa kuongoza au hawakuwa na nafasi tena ya kuwania uongozi ndani ya chama hicho katika uchaguzi ujao hawana nafasi.

Lakini pamoja na hayo, ni vyema chama hicho pia kikajikita katika kudhibiti rushwa ambayo imekuwa ikidaiwa kuwapo wakati wa kampeni za kura za maoni na kusababisha wagombea wasio chaguo kushinda.

Wakati huo ndio ambao wanachama huwa wanalalamika kuwa baadhi ya wagombea hupenyeza rupia ili kukubalika kwa wajumbe na kwa wananchi na hatimaye kuibuka washindi.

Hivyo, ili mkakati wa kuwaweka pembeni wagombea wasiokubalika na umma ufanikiwe, chama hakina budi kupenyeza watu wa kuwanasa wale watakaopenyeza rupia kwa lengo la kutaka wapitishwe kuwania uongozi.

Miaka ya nyuma katika kura za maoni, baadhi ya wagombea ndani ya chama waliwahi kulalamikia uwapo wa kadi mpya zilizokuwa zinatolewa kwa wasio wanachama ili wapige kura kumpa ushindi mgombea.

Vilevile, kulikuwapo na mtindo wa kutotumia daftari lenye orodha halali ya wanachama, badala yake kila aliyekuwa anafika sehemu ya kupigia kura, aliruhusiwa ili mradi ana kadi ya chama.

Baadhi ya viongozi wa chama wamekuwa wakituhumiwa kujihusisha na mchezo huo. Hivyo, wakati huu ambao CCM inakuja na mbinu mpya, ingeziba mianya hiyo ili lengo la kupata wagombea sahihi.

Kwa mfano, mwaka 2022, CCM ilisimamisha uchaguzi katika mikoa mitatu kwa nafasi zilizoonyesha kuwa na changamoto na kufuta uchaguzi wa Umoja wa Vijana wa CCM kwa sababu ya rushwa.

Hatua zilizochukuliwa na chama wakati huo za kufuta uchaguzi, zinaonyesha kuwa wagombea wasio na sifa huwa wanatumia njia isiyo halali kupata nafasi, hivyo, CCM haina budi kujipanga zaidi.

CCM ijipange kwa kuwafuatilia kwa karibu nyendo za watia nia, wajumbe na wanachama, ili kujiridhisha kama hakuna harufu ya rushwa ili hatimaye wapatikane wagombea ambao ni chaguo la wananchi.

Njia hiyo ikitumika inaweza kuja na matokeo chanya, kwani baadhi ya wanachama wanaodai kwamba, wakati wa uchaguzi wapo wenzao ambao husema hawako tayari kumpa mtu kura akale bila kuwapa chochote.

Wanaamini kwamba, wanapomchagua mtu katika nafasi ya uongozi, anakwenda kula, hivyo, wanaona ni bora nao wapate kitu kutoka kwa mgombea kuliko kumpa kura tu.

Hongera CCM kuwabana wagombea wakubebwa lakini ni vyema kama mtapenya kila kona kuwabaini wapigakura wa aina hiyo na wagombea wao, ili lengo la kupata viongozi wanaokubalika kwa wananchi litimie.

# Dar yaongoza kwa wananchi kutochukua vitambulisho NIDA

**Na Maulid Mmbaga**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA), imetoa angalizo hatua ya kusimamisha utaratibu wa watu kupatiwa huduma kwa kutumia namba za utambulisho (NIN), endapo wananchi wataendelea kupuuza kwenda kuchukua vitambulisho vyao ambavyo tayari vimeshatoka.

Kauli hilo imekuja baada ya kubainika kwamba kumekuwa na mrundikano mkubwa wa vitambulisho hivyo katika ofisi za serikali za mitaa, kata, vitongoji, vijiji, wilaya na mikoa, kutokana na wahusika kutokwenda kuvichukua, huku Mkoa wa Dar es Salaam ukitajwa kuongoza kutokana na wengi kutegemea kutumia namba walizopatiwa awali.

Akizungumza na Nipashe siku chache zilizopita Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano NIDA, Geoffrey Tengeneza, alisema kuwa Oktoba 2023, walianza uzalishaji mkubwa wa vitambulisho vya taifa na kuvisambaza kwa wingi katika maeneo mbalimbali katika mikoa, wilaya na vijiji.

"Yote hiyo ilikuwa ni kukidhi mahitaji ya wananchi ambao walikuwa wakilalamika hawana vitambulisho, kwasababu hatuzalishi hivyo wanakosa huduma, kwa hiyo tukaja na mkakati maalumu mkubwa wa kuzalisha 'mass production' na magari yakawa yanasafirisha usiku na mchana.

"Sisi tumefanya wajibu wetu kama mamlaka kwa kuzalisha kwa wingi na kusambaza ili wananchi wavichukue kutokana na mahitaji na kuondoa kelele za kwamba hawana vitambulisho, lakini kitu ambacho kimekuja kujitokeza watu hawajitokezi kwa kasi tuliyoitarajia ambayo ingeenda sambamba na kilio chao," alisema Tengeneza.

Alisema kuwa baada ya kusikia malalamiko ya wananchi walipata imani kwamba endapo watazalisha na kusambaza, ndani ya muda mfupi watajitokeza kwa wingi na kuchukua, akieleza kuwa kwa sasa hali ni tofauti na walivyotarajia kwa kuwa kasi ya wananchi sio kubwa hasa katika maeneo ya mijini.

Aidha, Mkoa wa Dar es Salaam uko chini kwa takwimu za kuchukua vitambulisho kuliko mingine yote, licha ya kuongoza kwa malalamiko ya watu kuonyesha uhitaji.

Alisema tatizo hilo linachangiwa na watu kuendelea kupatiwa huduma kwa kutumia namba za utambulisho wa taifa na kwamba hiyo inasababisha wananchi kutoona haja ya kwenda kuchukua kitambulisho hata kama anajua kuwa kimetoka.

"Tatizo lingine ni watu kuhama katika maeneo waliyojiandikishia ikiwamo watumishi wa umma na wanafunzi wa elimu ya juu ambao wameshamaliza masomo wamejiriwa katika maeneo mengine, huku nyuma vitambulisho vimetoka inakuwa shida kuja kuchukua.

"Kuna utaratibu wa kuchukuliwa kitambulisho mambo ya kuzingatia mhusika anatakiwa kuandika barua ya kumtambulisha atakayekwenda kumchukulia na ataweka sahihi yake, anaeenda kuchukua nae ataandika nyingine kwamba ataenda kumchukulia ndugu yake, ataandika majina yake, namba ya simu na kivuli cha namba ya utaifa," alisema Tengeneza.

Pia alisisitiza wananchi kuacha kisingizio cha kutokuchukua kitambulisho chake kwa sababu yuko mbali kwa kuwa mamlaka imeweka utaratibu mzuri wa kuchukuliana.

Awali, serikali iliweka utaratibu wa kila mwananchi awe na kitambulisho cha utaifa lengo likiwa ni pamoja na kuimarisha usalama na kuwa na taarifa muhimu za kila Mtanzania.

# TASAF yafanya mapinduzi sekta ya elimu, afya

**Faustine Feliciane na Restuta James**

MFUKO wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), umefanya mageuzi makubwa kwenye sekta ya elimu na afya kwa kuwezesha watoto 2,139,500 kutoka katika kaya maskini waliofikisha umri wa kwenda shule kuanza shule na 362,888 wanaotakiwa kuanza kiliniki wameanza kutokana na utekelezwaji wa mpango wa tatu wa kuzikwamua kiuchumi kaya masikini.

Akizungumza jijini Arusha jana, Mkurugenzi Mtendaji wa TASAF, Shedrack Mziray, alisema kuwa kabla ya utekelezaji wa mpango huo wa miaka mitano unaomalizika mwaka 2025, kulikuwa na pengo kubwa la watoto wanaofikisha umri wa kwenda shule au kupata huduma za kliniki wanashindwa kufanya hivyo kutokana na umaskini.

"Katika kipindi cha utekelezaji wa mradi huu wa kusaidia kaya maskini kujikwamua kiuchumi, watoto wengi walikuwa wakikosa mahitaji yao ya msingi, lakini katika kipindi cha utekelezaji mpaka kufikia Juni 2024, tumefanikiwa kupeleka shule watoto wenye umri kuanzia miaka sita mpaka 18, na wachanga kuanzia mwaka sifuri mpaka miaka mitano wameweza kuanza kuhudhuria kliniki," alisema Mziray.

Akifafanua, alisema katika kundi la watu wanaoweza kuzalisha mali, mfuko huo umewawezesha vijana kuanzia miaka 19 mpaka watu wazima wa miaka 59 kushiriki katika shughuli za kuzalisha mali, mpaka kufika mwezi Juni, mwaka huu watu 1,810,105 wamejiunga kwenye vikundi vya uzalishaji mali.

Aidha, alisema katika kipindi cha mradi, wamefanikiwa kuanzisha vikundi zaidi ya 60,000 vya uzalishaji mali kwenye kaya masikini ambavyo vinasaidia kuzalisha mali zinazosaidia kaya hizo kumudu maisha.

Alisema katika vikundi hivyo vilivyoundwa, vimekusanya zaidi ya Shilingi bilioni saba na kukopeshana Shilingi bilioni 3.2 ambazo zimewasaidia kubuni miradi mbalimbali ya kimaendeleo katika kaya zao.

"Manufaa ya mradi huu sasa hivi tupo mbioni kuziondoa kaya 400,000 kwenye kundi la wanufaika wa ruzuku za TASAF baada ya sasa kujimudu na kuendesha maisha yao bila kutegemea ruzuku tunazozitoa, hii italeta fursa sasa kuingiza kaya nyingine kunufaika na miradi ya mfuko," alisema Mziray.

**KAYA 697 ZAKWAMULIWA**

Kaya 697 zilizokuwa kwenye lindi la umasikini katika Manispaa ya Moshi, zimepewa 243,950,000, kwa ajili ya kuanzisha biashara ili wajitegemee kiuchumi.

Aidha, kaya 783 zilizokuwa kwenye umasikini uliokithiri zimefanikiwa kujitegemea kiuchumi.

Ofisa Ufuatiliaji wa TASAF Manispaa ya Moshi, Beatrice Shemdoe, aliyasema hayo jana mjini hapa wakati wa ziara ya waandishi wa habari kuwatembelea wanufaika wa fedha hizo.

"Katika kukuza uchumi wa kaya walengwa walishauriwa kuunda vikundi vya kuweka na kukopa ikafuatiwa na utoaji wa ruzuku ya uzalishaji mali. Kabla ya kupokea fedha, tuliwapa mafunzo ya kubuni na kuandaa mpango biashara," alisema.

Aidha, alisema kutokana na mafunzo walengwa 594 waliokuwa kwenye mpango wa TASAF walifanikiwa kuunda vikundi 48 katika Mitaa 34 ya Manispaa ya Moshi.

"Vikundi vyote vimewezeshwa na TASAF kwa kuwajengea uwezo kwa kuwapatia mafunzo viongozi wa vikundi, kuwapatia shajala na mabokși ya kuhifadhia nyaraka za kikundi," alisema.

Shemdoe alisema Manispaa hiyo ilikuwa na walengwa 1,566 wa TASAF ambao wamekuwa wakipewa fedha ya kujikimu kila baada ya miezi miwili.


Wakizungumza na waandishi wa habari mjini hapa, baadhi ya wanufaika walisema wamefanikiwa kulea watoto, kujenga nyumba na kuanzisha biashara ndogo.

Mnufaika Anna Msofe wa Mtaa wa KDC katika Kata ya Kibororoni, alisema kupitia TASAF amefanikiwa kujenga nyumba ya vyumba vinne kwa matofali ya kuchoma, na kuanzisha biashara ya ufugaji wa kuku na njiwa wa mapambo.

Aidha, alisema kabla hajaingia kwenye mpango wa TASAF alikuwa akiishi kwenye nyumba ya udongo na hakuwa na uhakika wa kipato.

"Nafuga njiwa tausi na njiwa simba. Kwa sasa ninao 50 na jozi inauzwa kati ya Sh. 250,000 hadi Sh. 300,000. Naishukuru sana TASAF kwa kuniwezesha," alisema.

Caroline Minja wa Mtaa wa Kariwa Chini, uliopo Kata ya Rau, alisema ruzuku ya uzalishaji mali, imemwezesha kufuga nguruwe na kufungua genge la vitu vya nyumbani.



Magistrates Court (Approved Forms for the Primary Court)

*GN. No. 943 (Contd.)*

*FOMU MADAI - 3*

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

MAHAKAMA YA TANZANIA

Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya KINONDONI

Kituo cha MAGOMENI Mkoa DAR ES SALAAM

Shauri la Madai/~~Ndoa~~ Na. 110/2024

Jina la mdai HALMASHAURI YA MANISPAA YA

Jina la Mdaiwa OMARI S. MUADI, JUSIANA Y. STANLEY, GLORY S. MANDARI

KUITWA SHAURINI MDAIWA

(*Kanuni ya 18 ya Kanuni za taratibu Madai Katika Mahakama za Mwanzo*)

Kwa OMARI S. MUADI, JUSIANA Y. STANLEY, GLORY S. MANDARI

Kwa kuwa Mdai/Wadai ameleta/Wameleta madai yake/yao kwamba (*Eleza hapa habari za Madai*) HKB MAHAKAMANI BILA KUKOSA ........ Kwa hiyo unatakiwa kuhudhuria binafsi katika Mahakama hii tarehe 22 Mwezi 7 Mwaka 2024 Saa 3:00 asubuhi/~~Mchana~~ kwa mujibu wa madai hayo na kwa kuwa siku hiyo ni siku ya kusikilizwa shauri hili ni lazima kuleta shahidi/mashahidi wako na vielelezo vyote vinavyohusu shauri hili kwa ajili ya kujitetea.

ANGALIZO: Kama hautohudhuria siku iliyotajwa hapo juu na ikithibitika kuwa ulipokea hati ya kuitwa shaurini, Mahakama inaweza kusikiliza shauri bila ya wewe kuwepo.

Hati hii imetolewa kwa Amri na Muhuri wa Mahakama hii leo tarehe 20 Mwezi 6 Mwaka 2024

HAKIMU

HAKIMU MKAZI MAHAKAMA YA MWANZO MAGOMENI - KINONDONI

PRIMARY COURT MAGOMENI DAR ES SALAAM TANZANIA

38

# DC akemea ung'oaji vibao anwani makazi

**Na Julieth Mkireri,** KISARAWE

MKUU wa Wilaya ya Kisarawe, Petro Magoti, amekemea vikali tabia ya baadhi ya wananchi kung'oa vibao vya anwani za makazi vilivyowekwa katika Kata ya Msimbu kwa madai kuwa maeneo hayo yako ndani ya Wilaya ya Ilala.

Aidha, alitoa wiki mbili kwa Ofisa Mtendaji wa Kata ya Msimbu pamoja na viongozi wengine wa kata hiyo kuainisha maeneo yaliyong'olewa vibao hivyo na waliohusika na vitendo hivyo wachukuliwe hatua za kisheria.

Magoti alitoa maagizo hayo mwishoni mwa wiki alipofanya mkutano na wananchi wa kata hiyo katika eneo la Majumba Sita ambao waliibua kero hiyo wakidai wapo watu wanang'oa baadhi ya vibao kwa madai maeneo hayo yapo ndani ya Mkoa wa Dar es Salaam, Wilaya ya Ilala.

"Yale sio mabango ya harusi au sendoff, serikali imetumia fedha nyingi kufanya kazi hii halafu anatokea mtu anaharibu, kama unataka toa nyumba yako sio kung'oa vibao vilivyowekwa," alisema Magoti.

Alipigia marufuku hiyo baada ya mmoja wa wananchi, Zakayo Samson, kuelezea katika mkutano huo kuwa vipo vibao vya makazi vinang'olewa na baadhi ya watu wakidai maeneo hayo yako Mkoa wa Dar es Salaam na sio Pwani.

"Moja ya kibao kilicho ondolewa ndani ya eneo la Homboza, kilikuwa cha shule na namba zinazofutwa ni zile za anwani za makazi na wanaweka na pia wanaweka wajumbe ndani ya eneo la mjumbe wa Homboza unakuta eneo moja kuna wajumbe wa Kisarawe na Ilala," alisema Zakayo.

Katika eneo hilo pia wananchi walieleza kuhusu kero ya barabara wakidai ya kiwango cha lami imejengwa hadi mpakani mwa Mkoa wa Dar es Salaam na Pwani na ukiingia Wilaya ya Kisarawe ni ya vumbi, huku ikiwa mbovu na kutopitika kwa urahisi kipindi cha mvua.

Akijibu hoja hiyo, Mkuu wa wilaya alibainisha kwamba ujenzi wa barabara hiyo umeanza baada ya Wakala wa Barabara za Mjini na Vijijini (TARURA), kupokea Sh. milioni 200.

# Mbowe alia madini tanzanite

**Na Godfrey Mushi,** ARUSHA

MWENYEKITI wa Taifa wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, amesema licha ya serikali kutumia mabilioni ya fedha kujenga ukuta kuzunguka vitalu vya machimbo ya tanzanite katika mji mdogo wa Mirerani, Wilaya ya Simanjiro, mkoani Manyara ili kudhibiti biashara haramu, madini hayo hayaonekani na kufifisha uchumi wa eneo hilo.

Aidha, amesema katika soko la dunia, tanzanite ambayo biashara yake kwa mwaka ni Dola za Marekani milioni 500, sawa na Sh. trilioni mbili, fedha hiyo haiinufaishi Tanzania, bali nchi nyingine tatu duniani ambazo hazizalishi madini hayo.

Akizungumza jana katika Jiji la Arusha, wakati akihitimisha operesheni +255 maarufu 'Operesheni GF' katika majimbo 35 ya mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Mbowe alisema, nchi hizo ndio zinazoongoza kwa kunufaika na tanzanite inayotoka Tanzania.

"Mirerani imekufa, kwa kudhibiti biashara ya Tanzanite. Magufuli (Hayati, Rais John Magufuli) amejenga ukuta wa mabilioni ya pesa yamepotea pale, tanzanite bado haionekani. Tanzanite inapatikana peke yake, hapo Manyara, hapo Simanjiro, Mirerani!

"Lakini kwenye soko la dunia, tanzanite ambayo biashara yake kwa mwaka ni Dola za Kimarekani milioni 500, kama karibu trilioni mbili. Hiyo pesa yote inakwenda India, Vietnam, Kenya.

Hizo nchi tatu ndio zinazoongoza kunufaika kwa tanzanite inayotoka Tanzania. Nchi zinazojitambua, serikali inajua ina wajibu, inafikiria itaajiri vipi vijana wake.

"Serikali inatakiwa kutengeneza mikakati ya kiuchumi na sera zitakazowezesha sisi kukua, kupanuka kwa haraka ili iweze kuajiri watu."

**LEMA ATETEA**

Mwenyekiti wa CHADEMA, Kanda ya Kaskazini, Godbless Lema alisema: "Leo tanzanite biashara imekufa, mabroka wa mawe (wanunuzi wadogo), leo wanaendesha bodaboda.

"Nenda pale kijiweni, mabroka wa mawe, ambao walikuwa ni mamilionea, leo wanakula mahindi 'lunch' mchana, hali imekuwa mbaya."

Kuhusu tatizo la ajira, Mbowe, alisema Tanzania hivi sasa inazalisha watoto milioni 1.6 kila mwaka ambao hawana ajira.

"Ni hivi, Watanzania kila mwaka darasa la saba wanamaliza hawaendi sekondari wanaingia mtaani soko la ajira. Wengine wanakwenda sekondari wanaishia kidato cha pili, kuna wanaoishia kidato cha tatu, kuna wengine wanamaliza kidato cha nne, kiasi kikubwa kinarudi mtaani, wengine wanaendelea mbele.

"Kidato cha sita wanamaliza hawaendi vyuo wanarudi mtaani, wa vyuo vikuu wanamaliza wanarudi mtaani. Tunazalisha watoto kwa mwaka sasa hivi milioni 1.6 kila mwaka.

Uwezo wa kutoa ajira katika uwezo wa Tanzania ya leo, una uwezo wa kuchukua watoto wasiozidi 300,000. Watoto milioni 1.3 wanarandaranda barabarani; wako wa vyuo vikuu, wako wa kidato cha sita, wako wa kidato cha nne, wako wa darasa la saba.

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TUME HURU YA TAIFA YA UCHAGUZI

## UZINDUZI WA UBORESHAJI WA DAFTARI LA KUDUMU LA WAPIGA KURA KATIKA MKOA WA KIGOMA

Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi inawatangazia wananchi wote kuwa Uzinduzi wa Uboreshaji wa Daftari la Kudumu la Wapiga Kura Awamu ya Kwanza utafanyika Mkoa wa Kigoma tarehe 20 Julai, 2024. Mgeni Rasmi katika uzinduzi huo atakuwa Waziri Mkuu Mhe. Kassim Majaliwa Majaliwa (MB). Siku hiyo ya uzinduzi ndiyo itakuwa siku ya kuanza kwa zoezi la uboreshaji wa Daftari Mkoani Kigoma, Tabora na Katavi kwa siku saba hadi tarehe 26 Julai, 2024.

1. **SIKU:** Uboreshaji utafanyika kuanzia siku ya Jumamosi tarehe 20 Julai, 2024 hadi siku ya Ijumaa tarehe 26 Julai, 2024
2. **VITUO:** Uboreshaji utafanyika katika vituo vilivyomo katika Mitaa, vijiji na vitongoji
3. **MUDA:** Vituo vitafunguliwa saa 2:00 Asubuhi na kufungwa saa 12:00 Jioni.

**Uboreshaji utahusisha: -**

1. Kuandikisha Wapiga Kura wapya ambao ni raia wa Tanzania waliotimiza umri wa Miaka 18 na zaidi na hawakuwahi kuandikishwa hapo awali.
2. Kuandikisha Wapiga kura ambao watakuwa wametimiza umri wa miaka 18 siku ya tarehe ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025.
3. Kuboresha taarifa za wapiga kura waliohama kutoka eneo moja kwenda eneo lingine la kiuchaguzi
4. Kutoa kadi mpya kwa wapiga kura ambao kadi zao zimepotea au kuharibika.
5. Kuboresha au kurekebisha taarifa za wapiga kura.
6. Aidha,Wapiga kura wanaotaka kuboresha taarifa zao na wanaohama kituo cha kupigia kura au vyote viwili wanaweza kuanzisha mchakato wa kuboresha kwa kujaza fomu maalum kwa njia ya mtandao kupitia tovuti ya Tume www.inec.go.tz au anuwani ya ovrs.inec.go.tz kwa kujaza namba ya kitambulisho cha Taifa, namba ya kadi ya mpiga kura, namba ya simu ya mpiga kura na jina la kata kisha watapokea ujumbe wenye namba ya utambulisho (token number) ambayo wataenda nayo kituo cha kujiandikisha ili kukamilisha taratibu na kupata kadi ya mpiga kura.

**MAMBO YA KUZINGATIA**

- Mwananchi anatakiwa kupanga mstari akiwa kituoni na kusubiri hadi zamu yake ya kuandikishwa itakapowadia. Watu wenye mahitaji maalumu kama vile wazee, wagonjwa, watu wenye ulemavu, wajawazito na akina mama wenye watoto wachanga watakaokwenda nao kituoni watapewa kipaumbele.
- Mwananchi atakapofika kituo cha kujiandikisha atachukuliwa alama za vidole vyote kumi vya mikono na kupigwa picha na kisha kupewa kadi yake mpya hapo hapo kituoni
- Ni muhimu kujiandikisha sasa katika Daftari la Kudumu la Wapiga Kura ili uweze kupiga kura katika Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2025 na chaguzi zijazo
- Zoezi hili halitawahusu wapiga kura ambao waliandikishwa awali, hawajahama maeneo yao ya kiuchaguzi na wana kadi zao za mpiga kura.

**KUJIANDISHA KUWA MPIGA KURA NI MSINGI WA UCHAGUZI BORA**

Limetolewa tarehe 27 Juni, 2024 na:

**Kailima, R. K.**
**MKURUGENZI WA UCHAGUZI**

# Wakulima wa migomba watakiwa kuzingatia haya

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAKULIMA wa migomba nchini wameshauriwa kufuata na kuzingatia kanuni bora za kilimo kwa kutumia mbegu sahihi, kuweka mbolea na kuhakikisha uwapo wa maji ya kutosha ili kupata mazao bora na kuleta manufaa ya kilimo.

Mkurugenzi Mtendaji wa kampuni inayojihusisha na kuuza bidhaa za kilimo na mifugo, Mrutu Agro-Solutions, Philipo Mrutu, alisema jana kuwa tatizo la migomba kutobeba kwa wakati inachangiwa na wakulima wenyewe kutofuata kanuni bora za kilimo na mgomba unapaswa uwe umeanza kuzaa unapofikisha miezi minane hadi mwaka mmoja tangu kupandwa.

"Wakulima wengi wamekuwa wakipanda bila kutumia mbolea, inawezekana mbegu wanayotumia kuwa sio nzuri na bora na suala la kumwagilia halipo, pia kama eneo halina mbolea inahitajika na suala la taratibu za upandaji linapaswa kuwapo kwa nafasi na kwa idadi ya mazao yanayotakiwa shambani kwa sababu mgomba hauwezi kumea na kuleta matunda kama hakuna vitu hivyo vitatu," alisema.

Mrutu alisema migomba kwa ajili ya uzalishaji inapaswa kwenye shina kutokuwa zaidi ya minne inayolingana bali inayopishana ili kutochukua chakula cha mwingine huku ikiwa haileti giza na kukosesha hewa kwenye mmea husika.

"Alisema mtu anaweza kuwa na migomba mingi na kupata tija kidogo sababu ya kutozingatia uzalishaji kwa eneo, mtu mwingine anaweza akawa na hekari moja halafu ana migomba 50 na kumbe anaweza kuwa na migomba zaidi na akapata matokeo mazuri zaidi na kuleta tija," alisema Mrutu.

Alisema matumizi ya mbegu bora inayoweza kuleta uzalishaji wenye tija kwa kuwa na ndizi zenye afya bila kuathirika ndio njia sahihi kwa sasa kwa wakulima na kwamba zipo mbegu zenye kuhimili magonjwa na ukame kama aina ya Fia 17 ambayo inaongoza kwa kuwa na toto (ndizi) mkungu mkubwa huku ikiwa na sifa ya kutoshambuliwa kwa magonjwa kwa urahisi.

Mrutu alisema zipo aina za mbegu za migomba 11 nchini ikiwamo aina mbili maalum ambazo ni machipukizi na njia ya maabara (Tissue Culture) ambayo ina mchakato mkubwa kidogo wa maandalizi.

Alizitaja aina 11 za mbegu za migomba zilizopo kuwa ni pamoja na mzuzu, kisukari, mkono wa tembo, mshale, malindi, bukoba, fia, bokoboko, uganda, mtwike na william.

Aliwataka wakulima kuwaona wataalamu wa kilimo ili wawatembelee kuangalia changamoto zinazowagusa kwenye suala zima la kilimo na kulipatia ufumbuzi kwa kupata mazao bora kwa maendeleo ya kilimo nchini.

Awali, mkulima mdogo wa migomba kutoka Kata ya Lukobe, Manispaa ya Morogoro, Dafrosa Rwegerela, aliwaomba wataalamu wa kilimo kuwasaidia katika uzalishaji wa migomba linalowasumbua na kujikuta wakikaa muda mrefu bila kuona faida ya zao walilopanda.

"Tuna migomba hapa sehemu kidogo tumepanda, sasa hata mvua inyeshe vipi hatuoni mazao na ikitokea imejaribu kuzaa basi inatoa kitoto kisichokuwa na afya, sasa hapa, natamani hata kuikata yote kwa kweli, kungekuwa na wataalamu labda tungejua sababu," alisema Rwegerela.



# H'shauri zajikongoja kutumia mamilioni kwa utapiamlo

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

HALMASHAURI za wilaya mkoani hapa hazijatumia ipasavyo kwa asilimia 100 fedha zilizotengwa kwa ajili ya kukabiliana na udumavu na utapiamlo kwa wakazi wake kipindi cha Januari hadi Machi mwaka huu.

Hayo yalisemwa na Ofisa Lishe wa Mkoa wa Manyara, January Dalushi, wakati akilielezea NIPASHE juu ya mwenendo wa fedha zilizotolewa kwa mkoa wao kukabiliana na udumavu na utapiamlo

Dalushi, alisema kwa kipindi hicho, Manyara imetumia kiasi cha Sh. milioni 444.232 kutekeleza afua za lishe kuanzia Januari hadi Machi mwaka huu kukabiliana na udumavu.

Alisema kiasi hicho ni kati ya Sh. milioni 514.802 sawa na asilimia 86 zilizotengwa na mkoa huo kutekeleza afua hizo ili kuhakikisha wakazi hao wanapata lishe bora.

Alisema fedha hizo zimetumika kwa kila halmashauri kulingana na takwa la kisheria ambalo linaitaka kutekeleza mkataba wa lishe ambao wakuu wa mikoa walisaini kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan ili waweze kusimamia utekelezaji na kuhakikisha fedha za lishe zinatengwa kwa watoto chini ya miaka mitano.

Alisema kwa kipindi hicho Halmashauri ya Wilaya ya Kiteto iliongoza kwa kutenga Shilingi milioni 94.198 na kutumia Shilingi milioni 91.4 sawa na asilimia 97.

Halmashauri ya Wilaya ya Mbulu ilifuatia kwa kutenga Shilingi milioni 65.3 na kutumia Shilingi milioni 62.7 sawa na asilimia 96.

Halmashauri ya Wilaya ya Hanang' ilitenga Shilingi milioni 91.154 na kutumia Shilingi milioni 80.0 sawa na asilimia 88, Mbulu Mjini ilitenga Shilingi milioni 36.7, ikatumia Shilingi mil.31.8 sawa na asilimia 87, Babati Mjini ilitenga Shilingi milioni 30.150 ikatumia Shilingi milioni 25.2 sawa na asilimia 84.

Simanjiro ilitenga Shilingi milioni 85.0 ikatumia Shilingi milioni 66.2 sawa na asilimia 78 na Halmashauri ya Wilaya ya Babati ilitenga Shilingi milioni 112.205 ikatumia Shilingi milioni 86.6 sawa na asilimia 77.

Mtaalamu huyo, alisema chanzo cha fedha hizo kubaki ni kulingana na miongozo, maeneo kutenga kidogo bila kufuata idadi ya watoto na waweka hazina wa halmashauri.

Juni 13 mwaka huu, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga akizungumza na waandishi wa habari, aliwaagiza watalaamu wa lishe kuongeza nguvu kudhibiti udumavu kwa kuwa mkoa una chakula cha kutosha na kuwaomba wazazi hasa wanawake kuona aibu ya watoto wao kudumaa.

Akizungumza na NIPASHE kujua mitazamo yao juu ya fedha hizo kutotumika, Mkazi wa Bagara Ziwani, Aron Daud, aliwataka waajiri kuwaadhibu wahusika kwa kushindwa kuwajibika ipasavyo kukabiliana na utapiamlo na udumavu.

Daud, alisema haiwezekani fedha zinatengwa kupambana na udumavu halafu hazitumiki zote kutokana na uzembe wa wachache.

Halima Hussen, aliiomba serikali kufuatilia taarifa za mapato na matumizi ya fedha za kila mtaa, kijiji na kitongoji.

Kwa mujibu wa Programu Jumuishi ya Taifa ya malezi makuzi na maendeleo ya awali ya mtoto ( PJT-MMMAM) ya mwaka 2021/22-2025/26, msisitizo wa lishe upo zaidi kwenye afua za lishe ya mama wajawazito, watoto wachanga na vijana.

## Jengo la upasuaji kujengwa KCMC

**Na Mary Mosha,** MOSHI

SERIKALI imetenga Shilingi bilioni 2 kwa ajili ya ujenzi wa jengo la upasuaji katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Mawenzi (MRRH) iliyopo mjini hapa Mkoa wa Kilimanjaro.

Hayo yalisemwa juzi na Mbunge wa Moshi Mjini, Priscus Tarimo, wakati wa uzinduzi wa gari jipya la wagonjwa na wa wodi ya upasuaji wanaume katika hospitali hiyo.

Tarimo, alisema kukamilika kwa ujenzi huo ni mwendelezo wa maboresho yanayofanywa na serikali kuhakikisha huduma bora za afya zinasogezwa karibu na wananchi.

"Ujenzi huu ni mwendelezo wa maboresho ya sekta ya afya yanayofanywa na serikali ya awamu ya sita nchini ya kujumuisha katika Mkoa wa Kilimanjaro kwa lengo la kusogeza huduma bora za afya karibu na wananchi," alisema.

Akizungumzia kuhusu gari hilo la wagonjwa lililozinduliwa hivi karibuni, Tarimo, alisema litasaidia kuboresha huduma za afya katika hospitali hiyo kwa kuzifanya kwa haraka.

Awali akitoa taarifa kwa mbunge huyo, Kaimu Mkuu wa Kurugenzi ya Upasuaji ya MRRH, Dk. Zawadi Mahumbuga, alisema wodi hiyo ya upasuaji ya wanaume itasaidia kupunguza msongamano wa wagonjwa hospitalini hapo.

"Hapa tunapokea takribani wagonjwa 60 kila mwezi, ambao wanahitaji upasuaji wengi wao ni wale wanaopata ajali, wodi hii mpya itasaidia kupunguza ya ongezeko la idadi ya watu, ingawa mahitaji ya wodi nyingi bado yapo," alisema.

Daktari Mfawidhi wa hospitali hiyo, Dk. Edna-Joy Munisi, alisema kuzinduliwa kwa wodi hiyo kumeweka mazingira bora kwa watoa huduma na wapata huduma.

"Tutajumuisha huduma kwa wagonjwa wote wa mifupa, macho, kinywa, pua, masikio na koo ambazo zitakuwa za kibingwa," alisema.

Alisema wanatarajiaa kuanzisha huduma ya kusafisha damu kwa wagonjwa hospitalini hapo.

"Tunaishukuru serikali kwa kutenga zaidi ya shilingi milioni 300 katika ujenzi unaoendelea wa miundombinu ya huduma ya kusafisha damu," alisema.

Alitaja maendeleo mengine katika hospitali hiyo ni ujenzi wa tanuru la kuchoma vifaa hatari katika hospitali hiyo.

## Nchi EAC zapewa somo utunzaji mazingira

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKURUGENZI wa Taasisi ya Masomo ya Tabia nchi na Mazingira wa Chuo Kikuu cha Aga Khan Tawi la Arusha, Dk. Emmanuel Sulle amezitaka nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) kuongeza viwanda vya kuzalisha bidhaa zisizoharibu mazingira na kufyonza kaboni kwa Maendeleo Endelevu (SDGs).

Dk. Sulle aliyasema hayo juzi katika tawi hilo wakati akizungumza na waandishi wa habari kuhusu umuhimu wa kuhifadhi mazingira ili kuwalinda binadamu, mimea na mifugo na madhara ya mabadiliko ya tabia nchi.

Alisema endapo nchi za zikiongeza zaidi viwanda vinavyozalisha bidhaa zisizoharibu mazingira, wananchi watanufaika na ajira, utunzaji wa miti utakaowezesha uvunaji wa bayonuwai na kufyonza kaboni ili kulinda mazingira.

"Taasisi yetu imejikita zaidi katika kutatua changamoto za mazingira, hasa zinazoathiri jamii zinazoishi ukanda wa Kaskazini mwa Tanzania, kutokana na ukame unaoletwa na mabadiliko ya tabia nchi, hivyo tunashauri jamii za maeneo hayo kupanda miti na majani inayohimili ukame, pia wanapata malisho na kuinua uchumi wao.

"Lakini mbali na kupata malisho wanahifadhi mazingira yao kwa sababu yanasaidia kuzuia mmomonyoko wa udongo," alisema Sulle.

Alisema katika karne ya sasa, elimu ya kukabiliana na mazingira si ya kukaa darasani pekee, lazima wanafunzi watekeleze kwa vitendo ili kuhakikisha mazingira yanatunzwa.

"Kutokana na taasisi yetu kujua hili tunashirikiana na jamii kwa kupata maarifa asili katika utunzaji wa mazingira ikiwemo mifugo, lakini tunapokea wanafunzi wa vyuo vikuu ndani na nje ya nchi kuja kujifunza hapa kwetu kwa vitendo utunzaji wa mazingira," alisema.

Vilevile, alisema taasisi hiyo ina miti zaidi ya 100 ya aina tofauti, ikiwemo mpingo ambayo ina thamani kubwa nchini.








# DPP, washtakiwa uporaji dhahabu wakubaliana

**Na Samson Chacha,** TARIME

WASHTAKIWA nane wa kesi ya utakatishaji na ufadhili wa waporaji wa mawe ya dhahabu katika Mgodi wa Barrick North Mara wameingia makubaliano na Mkurugenzi wa Mashtaka nchini (DPP) kulipa Sh. milioni 62.5 kila mmoja ili kumaliza shauri hilo.

Kufuatia makubaliano hayo, washtakiwa watatu kati yao, wamelipa Sh. milioni 94.5.

Awali akiwasomea mashtaka katika Mahakama ya Wilaya ya Tarime mbele ya Hakimu Mkazi Stanley Mwakihaba, Mwendesha Mashtaka wa Serikali, Devis Katesigwa na wenzake kutoka Ofisi ya DPP alidai kuwa washtakiwa hao, wanakabiliwa na kesi ya utakatishaji na kuwa mawakala wa kufadhili waporaji wa mawe ya dhahabu katika mgodi huo na kuyanunua kwa njia zisizo rasmi.

Katesigwa alidai kuwa washtakiwa hao walitenda makosa hayo Mei 29, mwaka 2023. Alisema mshtakiwa Abia Sasi (48), amelipa fedha yote kulingana na makubaliano yake na DPP wakati Raphael Matiko na Makenge Chacha wamelipa Sh. milioni 32.

Aliwataja washtakiwa watano ambao bado hawajalipa chochote kuwa ni Emmanuel Joseph maarufu kwa jina la Stemina , Ghati Bare, Hamis Maiko, Chacha Mwita na Mang'era Chacha.

Alisema washtakiwa wengine, Yohana Chacha na Ketabo Ryoba wameonywa na kuwekwa chini ya uangalizi wa Jeshi la Polisi kwa kipindi cha mwaka mmoja.

Washtakiwa hao wametakiwa kuripoti Kituo cha Polisi Nyamwaga kila mwezi, kutojihusisha na kushawishi vijana kuvamia mgodi na kununua mawe yanayosadikiwa kuwa na dhahabu yaliyoporwa mgodini.

Hakimu Mwakihaba aliahirisha kesi hiyo hadi Julai 22, mwaka huu, itakapotajwa tena na kuwahimiza washtakiwa waliosalia kulipa faini hiyo kulingana na makubaliano yao na DPP.



Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Anamringi Macha akizungumza kwenye kikao cha bodi ya barabara juzi na kuonyesha kukerwa na makandarasi wenye uwezo mdogo kupewa kazi ya kutengeneza miondombinu ya barabara na kushindwa kuikamilisha kwa wakati huku wengine wakiwa hawapo kabisa eneo la mradi na hawana vifaa vya ujenzi. **PICHA: MARCO MADUHU**

# Waganga walia kamata kamata ya Polisi Ushetu

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

WAGANGA wa jadi katika Halmashauri ya Ushetu mkoani Shinyanga, wameiomba serikali kuingilia kati ili wapate haraka vibali na kuwaondelea adha ya kukamatwa mara kwa mara na askari wa Jeshi la Polisi.

Wametoa ombi hilo wakati wakiwasilisha malalamiko kwenye mkutano na Mbunge wa Ushetu, Emmanuel Charahani.

Waganga hao walidai kuwa licha ya baadhi yao kulipia vibali hivyo kwa muda mrefu, hawajapatiwa hali inayosababisha waendelee kukamatwa na askari hao kwa tuhuma za kufanya kazi zao kinyume na sheria.

Mganga wa Nyamilangano Makolo Bundala, alidai kwa zaidi ya miaka miwili amelipia kibali chake, lakini mpaka sasa hajapata.

Bundala, alisema licha ya kulipia kibali hicho kupitia namba ya malipo ya serikali, kila siku amekuwa akikamatwa na askari hao kwa kushirikiana na ofisa utamaduni na kutozwa faini.

Alimuomba mbunge huyo kuingilia kati kuhakikisha vibali hivyo vinapatikana kwa wakati baada ya kulipia na kuwaondolea gharama kwa kutozwa faini na matumizi mengine ya fedha.

Ramadhani Nkina, alidai wamekuwa wakikamatwa na silaha za jadi ambazo wamerithi kwa baba zao na kubambikiwa kesi ya kuwinda wanyama.

Mratibu wa Tiba Asili wa Halmashauri ya Ushetu, Allec Silayo, alikanusha madai ya waganga hao na kusema wengi wao wanatumia vibali vya kughushi.

Silayo, aliwataka waganga hao kufika katika ofisi zinazohusika kusajili shughuli zao, ikiwemo nyara wanazozitumia ili kuondokana na usumbufu huo.

Mbunge Charahani aliahidi kufikisha malalamiko ya waganga hao katika mamlaka husika na bungeni ili kubaini sababu ya vibali hivyo kuchelewa kuwafikia na kuhakikisha wanafanya kazi zao bila kubughudhiwa na jeshi hilo.

Hata hivyo, aliwataka kwa kipindi ambacho anashugulikia malalamiko yao, wajiepushe na tabia ya kugushi vibali kwani vinasababisha serikali kupoteza mapato.

Aliwataka wenye nyara ambazo hazijasajiliwa wahakikishe wanazisajili ili kuondokana na adha za kukamatwa mara kwa mara.

# Katambi awaangukia wazee maadili kwa vijana

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WAZEE wa Manispaa ya Shinyanga wameombwa kukabiliana na mmomonyoko wa maadili kwa vijana kwa manufaa yao na taifa.

Ombi hilo limetolewa na Mbunge wa Shinyanga Mjini, Patrobas Katambi ambaye pia ni Naibu Waziri Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na watu wenye ulemavu.

Katambi alitoa ombi hilo juzi wakati akizungumza na wazee hao na kuzindua Umoja wa Wazee Wastaafu Tarafa ya Oldshinyanga.

Alisema tatizo hilo kwa vijana limekuwa kubwa, hivyo wazee kusimama ni wajibu wao wa msingi kwa kulipigia kelele na kulikemea ili kuliokoa taifa.

"Vijana ndiyo nguvu kazi ya Taifa, sasa wakianza kuoana wanaume kwa wanaume, wanawake na wengine kupenda kuwa ma "single mother" taifa linakwenda kuangamia na kuna uwezekano hata hapo baadae kuja kukosa viongozi wazuri wenye maadili, sababu ya kuathiriwa na mmomonyoko wa maadili," alisema.

Aliwaomba wazazi kuacha malezi ya kisasa kwa watoto ambayo ndiyo yamekuwa chanzo cha mmomonyoko wa maadili kwa vijana.

Aliwataka warudi katika malezi ya enzi za mababu ili kuwafanya watoto wakue katika maadili mema.

Mwenyekiti wa Baraza la Ushauri la Wazee Manispaa ya Shinyanga, Stephano Tano, alimshukuru mbunge huyo kwa kukutana na wazee na kuiomba serikali kuwapatia vitambulisho vya matibabu bure na dawa.

Tano, alisema ajenda kubwa ya wazee kwa sasa kwenye vikao vyao ni kujadili namna ya kuanza kutoa elimu dhidi ya mmomonyoko wa maadili kwa vijana.

**Aliwaomba wazazi kuacha malezi ya kisasa kwa watoto ambayo ndiyo yamekuwa chanzo cha mmomonyoko wa maadili kwa vijana.**

Ukurasa 12



**Nukuu ya Nyerere inapotumiwa kukimbia vyama, Msigwa aitaja**

Ukurasa 13



**Tume Uratibu Dira, sikieni jambo la wanawake hawa**



# Msajili ndani ya mgogoro wa TLP, kuufumua sasa

• Katibu ashangilia mkwamo akidai hakuna uchaguzi ni 'kicheni pati'

**Na Sabato Kasika**

MGOGORO wa kiuongozi ndani ya Chama cha Tanzania Labour Party (TLP), huenda ukapata ufumbuzi baada ya Ofisi ya Msajili wa Vyama Siasa, kupanga kuushughulikia kuanzia leo.

Chama hicho kimekumbwa na mgogoro baada ya kuitisha uchaguzi lakini ukakataliwa na Ofisi ya Uchaguzi kwa maelezo kuwa haikuwa na taarifa.

Hata hivyo, ndani ya chama wapo wanaunga mkono uchaguzi wa Mwenyekiti wa Taifa, Aivan Maganza, na wengine wanampinga hivyo kusababisha kuwapo makundi yanayovutana baada ya uchaguzi huo uliofanyika mwezi uliopita Juni 29.

Makundi hayo ni lile linamuunga mkono makamu mwenyekiti wa chama hicho, Dominatha Rwechungura na katibu aliyeondolewa katika nafasi hiyo baada ya uchaguzi, Richard Lyimo.

### KUTEGUA KITENDAWILI

Akizungumza na gazeti hili jijini Dar es Salaam jana, Msajili Msaidizi wa Vyama vya Siasa, Sisty Nyahoza, anasema mgogoro huo umeifikia ofisi yao.

Anafafanua kuwa wamepokea taarifa ya uchaguzi huo kutoka kwa Makamu Mwenyekiti TLP Taifa, Dominatha Rwechungura.

"Baada ya kuletewa taarifa za kufanyika uchaguzi wa mwenyekiti wa TLP taifa, tuliwasiliana na katibu mkuu wa chama, Richard Lyimo kupata maelezo zaidi kuhusu uchaguzi," anasema Nyahoza.

Nyahoza anafafanua kuwa Lyimo aliwaambia kwamba hana taarifa yoyote kuhusu chama kufanya uchaguzi.

"Baada ya majibu hayo, tumemwandikia katibu huyo barua atoe maelezo kwa nini upande mmoja unasema uchaguzi ilifanyika na mwingine unakana kufanyika uchaguzi," anasema.

Anasema, Lyimo anatakiwa kupeleka maelezo haraka ili leo Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa itoe majibu ya hatima ya mgogoro wa kiuongozi ambao umejitokeza ndani ya chama hicho. Anasema, kwa kawaida chama kinapomaliza kufanya uchaguzi, ni lazima kipeleke taarifa katika Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa ili kupitia taarifa za uchaguzi huo.

"Hao walifanya uchaguzi wameleta taarifa zao tuzipitie tujiridhishe kwanza ili kuepusha migogoro ya kiuongozi ndani ya vyama," anasema.

### M/KITI APIGWA STOP

Tangu kufanyika kwa uchaguzi huo uliompa ushindi Aivan Maganza, mwenyekiti huyo mpya wa TLP hajaingia ofisini kutokana na kile anachoeleza kuwa ni kuzuiwa na walinzi wa makao makuu ya chama hicho.

Maganza anasema, baada ya kumalizika uchaguzi, Julai mosi aliripoti ofisini akiwa na safu mpya ya uongozi, akiwamo katibu mkuu mpya Riziki Ngaga.

"Lakini tulipofika tulizuiliwa na walinzi kwa maelekezo ya Lyimo na hadi sasa tumeshindwa kufanya kazi za chama kwa sababu ya mtu mmoja anayevuruga mambo," anadai Maganza.

Anasema, Lyimo alipata nguvu baada ya kuwapo taarifa kuwa Ofisi ya Msajili wa Vyama vya Siasa haitambui uchaguzi huo, na kwamba walipeleka vielelezo vyote vya uhalali wa uchaguzi katika Ofisi ya Msajili.



Makamu Mwenyekiti TLP, Dominatha Rwechungura akizungumza kuhusu mikakati ya chama. **PICHA: SABATO KASIKA**

"Kwa kuwa ofisi hiyo imepokea vielelezo, tunaamini itatenda haki katika maamuzi yake, kwa sababu hatukufanya uchaguzi kwa kificho, ofisi ya msajili inajua, Jeshi la Polisi linajua, ndio maana lililinda uchaguzi wetu," anasema.

### KICHENI PATI

Akizungumzia tuhuma zinazoelekezwa kwake, Lyimo anasema, ni kweli amewazuia wasiingie ofisini, kwa maelezo kwamba chama hakijafanya uchaguzi.

"Kilichofanyika ni 'kicheni pati' sio uchaguzi, kwa sababu uchaguzi hauwezi kufanywa na wajumbe tisa. Hao ni wahuni tu," anasema Lyimo.

Anaongeza kuwa uchaguzi kama huo ni lazima katibu mkuu na kaimu mwenyekiti wa chama taifa wawepo, na kwamba yeye na kaimu mwenyekiti hawakuwapo.

"Kwa hiyo nirudie kusema kuwa hao watu walifanya 'kicheni pati' sio uchaguzi, kwa hiyo hatuwatambui kama viongozi bali ni wahuni tu," anasema.

### UCHAGUZI ULIVYOKUWA

Katika uchaguzi huo, wajumbe wa mkutano mkuu walimchagua Maganza kuwa mwenyekiti wa chama hicho taifa kwa kura 35, huku Stanley Ndamugoba alipata kura 10, Kinanzaro Mwanga kura 10, Abuu Changaa kura sifuri na Richard Lyimo kura sifuri.

Hayo ni kwa mujibu wa makamu mwenyekiti wa chama, Dominatha Rwechungura ambaye anafafanua kuwa baada ya uchaguzi, halmashauri ilimchagua Riziki Ngaga kuchukua nafasi ya Lyimo aliyeondolewa katika nafasi hiyo na kubaki mwanachama wa kawaida.

"Lakini mwanasiasa mkongwe Hamad Tao, alichaguliwa naibu katibu wa chama chetu. Hao ndio baadhi ya viongozi wa juu wa TLP," anasema.

Uchaguzi huo ulifanyika baada ya kuahirishwa kwa zaidi ya mwaka mmoja huku ikielezwa kuwa chanzo cha hayo ni baadhi ya viongozi kung'ang'ania madaraka.

Mara ya kwanza, chama kilipanga kufanya uchaguzi Januari 8 mwaka jana, lakini ukaahirishwa hadi Machi 6, lakini haukufanyika ukapanguliwa hadi Mei mosi mwaka huo wa 2023.

Hata hivyo, uchaguzi huo pia haukufanyika ukasogezwa mbele hadi Desemba 28 mwaka jana, lakini ukaahirishwa ukapangwa kufanyika Januari 28, mwaka huu, nao ukapigwa kalenda.

Baada ya panga pangua hiyo, hatimaye ukafanyika Juni 29, lakini ili kuziba nafasi ilioachwa na Augustine Mrema aliyefariki dunia Agosti mwaka 2022, lakini nao umekumbwa na sintofahamu baada viongozi waliochaguliwa kuzuiwa kuingia ofisini.

# Nukuu ya Nyerere inapotumiwa kukimbia vyama, Msigwa aitaja

## •Ni ile 'CCM siyo mama yangu'



Rais Samia Suluhu Hassan, akimkaribisha Peter Msigwa, baada ya kukihama chama chake cha CHADEMA. **PICHA: MTANDAO**

**Na Restuta James**

IMEKUWA ni kawaida kwa wanasiasa kuhama kutoka chama kimoja kwenda kingine, hasa nyakati za uchaguzi, wengi wakihalalisha uamuzi wao na tuhuma za kutoridhishwa na baadhi ya mambo kule wanapokokimbia

Wachambuzi wa siasa wanaeleza kuwa ili mtu ajiunge na chama kwanza lazima akubaliane na itikadi au msimamo wa chama anachokitaka katika masuala yote ya msingi hususani namna ya kushika dola, usimamizi wa uchumi na rasilimali za nchi na muundo wa taasisi za umma hasa majeshi.

Wanadokeza kuhusu itikadi wakizitaja zipo zinazoamini katika mrengo wa kulia, wa kushoto, wa kati, kati kulia, kati kushoto, ujamaa na ukoministi.

Itikadi hizi zinaelezwa kuwa ndio msingi wa mwananchi kuamua kujiunga na chama kwa kuwa ndio imani yake kwa kile anachotaka kukiona kesho kwa nchi yake.

Mwanasiasa mkongwe, Thomas Ngawaiya, anasema ni vigumu kwa mwanasiasa makini kuhama kutoka chama kimoja hadi kingine kwa kuwa imani ya itikadi inambana.

"Ukiona mtu anahama chama ujue hakuna kitu kingine kinachomsumbua zaidi ya ubinafsi na wanasiasa wengi wanaangalia zaidi maslahi yao na sio kusaidia umma. Binafsi nalichukia jambo hili kwa sababu linarudisha nyuma malengo ya jamii," anasema.

Anafafanua kuwa ubinafsi wa wanasiasa umekwamisha malengo ya kuanzishwa kwa mfumo wa vyama vingi.

"Lengo kubwa la chama cha siasa ni kuwaletea wananchi maendeleo pale wanapopewa nafasi ya kuongoza kutokana na itikadi yake, ukifuatilia wanaohama ni kwa sababu wamekosa nafasi kwenye uchaguzi ndani ya chama au kutoteuliwa kuwania nafasi kama za urais au ubunge;"

Anasema na kuongeza kuwa nia yake anayehama ni kuingia kwenye nafasi fulani sio kuisaidia jamii katika kile wanachoamini.

Ngawaiya ambaye aliwahi kuwa mbunge wa Moshi Vijijini akianzia NCCR-Mageuzi na kisha kuhamia TLP na sasa yuko CCM, anasema hakutaka kuhama lakini mazingira yalimlazimisha baada ya kugombana na aliyekuwa Mwenyekiti wake, marehemu Augustino Mrema, hadi kufikishana mahakamani.

"Siungi mkono kuhamahama vyama. Ni kikwazo kwa jamii ambayo inaamini pamoja na wewe kwenye itikadi, ghafla unabadilika. Ndio maana nasema kama si ubinafsi, kuhama chama ni jambo gumu kwa mtu makini," anaongeza.

**CCM SI MAMA**

Akizungumza na Nipashe, aliyewahi kuwa Mbunge wa Iringa Mjini (CHADEMA), Peter Msigwa, ambaye karibuni amehamia CCM, anasema suala la itikadi kama msingi wa imani ndani ya chama cha siasa ni jambo jepesi linaloweza kubadilika wakati wowote.

"Kwani hukumsikia Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere akimwambia Kawawa CCM sio mama wala baba yake?" Itikadi sio dini wala sio imani ni jambo linaloweza kubadilika wakati wowote," anasema.

Anaahidi kujibu swali hilo kwenye mkutano na waandishi wa habari ambao hata hivyo hajaufanya.

CHADEMA Msigwa aliyoikimbia, inaamini katika itikadi ya mrengo wa kati wakati CCM alikohamia inaamini katika siasa za ujamaa na kujitegemea, japo kinachoonekana ni uelekeo wa mrengo wa kulia lakini pia kushikilia jukumu la serikali kusimamia maendeleo.

Itikadi inatafsiriwa na kutokana na mambo ambayo chama huyaamini, kuyasimamia na kuyapigania kama ajenda zake za msingi kwa wananchi na taifa kwa ujumla.

**ITIKADI CCM/CHADEMA**

Pamoja na kwamba wanasiasa nchini wanahama kutoka kila upande, vyama vya CCM na CHADEMA vinaongoza kwa makada wake kuhamia upande mwingine na wakati mwingine kuunda vyama kama ilivyotokea wakati wa awamu ya nne, baadhi ya makada wa CCM walivyoasisi kuanzishwa chama cha kijamii (CCK) na msuguano ndani ya CHADEMA ulivyozaa ACT-Wazalendo miaka 10 iliyopita.

Hata hivyo, CCM inaamini katika itikadi ya ujamaa na kujitegemea ambayo ilipewa nguvu ya kisera na Azimio la Arusha ambalo liliweka uchumi mikononi mwa umma.

Itikadi hiyo ilisisitiza umuhimu wa kuishi pamoja jambo lililoanzisha vijiji vya ujamaa na kuimarisha vyama vya ushirika.

Falsafa ya CCM inasisitiza kuzingatia utu, usawa na haki; inayosimamiwa na siasa safi na uongozi bora ili kudumisha amani, umoja na mshikamano wa kitaifa.

Kwa upande wa CHADEMA, inaamini katika mrengo wa kati kikiongozwa na falsafa ya 'nguvu na mamlaka ya umma' au The People's Power' katika kumiliki, kuendesha, kubuni na kuendeleza maamuzi, mawazo, rasilimali, uchumi na siasa ya nchi.

**UFAFANUZI KIMRENGO**

Vyama vyenye mrengo wa kushoto vinaamini katika usawa, ushirikiano, kusaidiana na kuwasaidia wasiojiweza, uhuru wa kujitawala, haki na fursa za kisiasa na kiuchumi kwa mwanamke, mgawanyo bora wa kodi, bima za afya kwa umma sambamba na haki na usawa kwa wafanyakazi.

Vyama hivi vinasikiliza na kuamini katika maslahi ya msingi ya wananchi wao, mfumo wenye usawa katika uongozi, matajiri wawasaidie masikini na athari za mabadiliko ya tabianchi.

Vyama vyenye mrengo wa kushoto vipo kinyume na aina yoyote ya ukandamizaji, ubaguzi wa rangi ama unyanyasaji wa kibinadamu.

Kwa upande wa mrengo wa kulia vinaamini katika utamaduni wa asili wa dola kama vile kuwa na jeshi kubwa, silaha kali na kupigana vita kwa ajili ya kulinda na kutetea maslahi yao, utaifa na dola kwanza na ulinzi na usalama wa dola.

Vyama hivi vinaongozwa na itikadi kuwa dola linapaswa kuhakikisha linapambana na vitisho vyote vya ndani na nje ili kuhakikisha linaendelea kuwepo.

Vyama nyingine vya mrengo wa kulia vinaamini pia kuwa nchi zinapaswa kulinda maslahi yao ya kibiashara, hata kwa kuweka vikwazo wakati fulani.

Vyama vyenye mrengo huu huwa haviamini sana katika ushirikiano na hata vinapokuwa madarakani mahusiano baina ya nchi na nchi huyumba.

Kwa upande wa Uingereza vyama vyenye itikadi ama mrengo wa kulia ni Conservative kilichoshadidia kujitoa kwa Uingereza Umoja wa Ulaya-wakiita hatua hiyo British exit au Brexi, hatua ambayo imekuwa na changamoto nyingi kiuchumi na kijamii.

Kwa Marekani Republican kinachokusudia kumteua Donald Trump kuwa mgombea urais kinaongozwa na mrengo huo na mara nyingi hakiwajali maskini wakiwamo weusi na kinaendeleza ubaguzi.

**MRENGO WA KATI**

Vyama vyenye mrengo wa kati vinayaamini mambo yote yanayosimamia itikadi za mrengo wa kulia na wa kushoto kwa pamoja kwa umuhimu wake ikiamini katika ustawi wa nchi na dunia.

Mfano wa vyama hivi ni chama cha Liberal Democrats cha Uingereza ingawa kuna wakati nacho huonekana kuegemea siasa za mrengo wa kulia.

CHADEMA ndicho kinachoamini katika itikadi hii kwa maana kwamba kinaangalia mambo yanayofaa kwenye mirengo yote miwili na kuyasimamia huku kikipinga baadhi ya mambo pia.

Vyama vyenye mrengo wa kati kushoto vinaamini yale ya mrengo wa kushoto huku yale ya mrengo wa kulia wakiyakubali kwa kiasi fulani.

**MRENGO KATI, KULIA**

Kama ilivyo kwa mrengo wa kati kushoto, vyama vyenye mrengo wa kati kulia vinaamini zaidi yale ya mrengo wa kulia lakini pia huyatilia umuhimu yale ya mrengo wa kushoto.

# Tume Uratibu Dira, sikieni jambo la wanawake hawa

Na Mwandishi Wetu

"TUNAFURAHIA dira ya maendeleo ya taifa 2050, jinsi ilivyo shirikishi na jumuishi inayokusudia kumfikia kila mmoja, aeleze Tanzania anayoitamani. Ni jambo la kihistoria."

Anasema Mwenyekiti wa Jumuiya ya Wanawake Wenye Ulemavu Zanzibar (JUWAUZA), Salma Haji Sadat, akizungumza na Nipashe baada ya kongamano la kitaifa la wanawake kuchangia maoni ya Dira ya Taifa 2050, mwishoni mwa wiki iliyopita.

Kongamano hilo linaloandaliwa na Mfuko wa Udhamini wa Wanawake (WFT), Mtandao wa Jinsia Tanzania (TGNP) na Shirika la Wanawake katika Sheria na Maendeleo Afrika (WiLDAF) linawakutanisha wanawake na wajumbe wa Tume ya Mipango na Uratibu wa Dira ya Taifa, Dar es Salaam.

Salma, anasema ni dira jumuishi yenye mawazo ya wengi na mambo bora ambayo yakiwekwa kwenye vipaumbele vya taifa huenda yakaleta Tanzania bora zaidi hata kabla ya kufikia 2050.

Hata hivyo, ana angalizo kwa Tume ya Kuratibu Maoni ya Dira kuwa Tanzania lazima ikomeshe rushwa na kufanya mikakati ya kupata fedha za ndani kuendesha miradi ya maendeleo na ujenzi wa nchi.

Anatamani dira inayoondoa rushwa ili mamilioni ya pesa za miradi yanayoibwa kila mwaka yasichotwe yatumiwe kuondolewa wananchi umaskini.

Aidha, dira inayolinda na yenye uchungu na rasilimali za nchi ili zisiporwe na kumalizika badala yake zilete maendeleo kwa kila mmoja.

"Rasilimali ziwape watu maji safi, umeme, elimu bora, barabara za kutosha, chakula na fedha wasilie hali ngumu na umaskini".

Salma anagusia elimu, kuwa dira iifikishe Tanzania kwenye elimu bora si kukariri maandiko badala yake wajifunze zaidi mambo ya kukuza na kuendeleza kada (professions) kama ualimu, uhandisi, kilimo na uandishi wa habari, akisema ndivyo wanavyofanya China na mataifa ya Korea, Malaysia na Indonesia.



Mwenyekiti wa JUWAUZA , Salima Haji Sadat.

**VIJANA KAA LA MOTO**

Salma Mwenyekiti wa Baraza la Taifa la Watu Wenye Ulemavu Zanzibar, anagusia utitiri wa vijana usiona na tumaini, akisema ni kundi kubwa zaidi na linaloendelea kuongezeka kila siku kwa idadi, hivyo serikali ifanya kila mbinu kutatua kero zao maana wako nyuma zaidi.

Anashauri iwekwe mikakati yenye kuleta mabadiliko ya haraka ili kubadili maisha yao maana ni wengi wakiachwa bila ajira, elimu, mikopo, misaada wala kuendelezwa wanaweza kuwa changamoto kubwa kwenye taifa.

"Tutumie teknolojia na maarifa kuwawezesha kubadili maisha yao, wawe na kazi wapate fedha, waingizwe kwenye kilimo, ufundi na teknolojia ili kuwanyanyua kwani ni kundi kubwa, liangaliwe kwa jicho pevu." Anaeleza.

Pili Kuliwa ni Mratatibu wa Shirika la Tumaini Jipya la Wanawake Kilwa (TUJIWAKI), anasifu dira shirikishi inayowapa wengi nafasi ya kutoa maoni yao kuanzia mikaoni, mijini, vijijini, akisema haijawahi kufanyika tangu uhuru.

Anataka dira iangalie ulinzi wa watoto Bara na Visiwani kwa sababu wanatelekeza, kuwaacha watunzwe na ndugu au wazee wasio na kipato na wengine kuishi kwenye mazingira magumu na ya kihalifu, ngono na dawa za kulevya.

Anaeleza kuwa kuna kizazi cha watoto wengi wenye umri wa chini ya miaka 15 ambao hawasomi, wasio na malezi, waliofanyiwa ukatili ambao wamesambaa karibu kila mahali.

"Tusipofanya hivyo ikifikapo 2050 tutakuwa na vijana wengi wasiojua kusoma kabisa, wasiojitambua, wahalifu ambao ni mzigo usiobebeka kwa taifa."

Mkurugenzi wa Chama cha Solidarity for Women and Children with Disabilities (SOWACHIDI), Adeline Mluge, anasifu ushirikishwa wa wananchi kuandaa dira akitaka ifanyike tathmini ya upungufu na kasoro za kutekeleza dira 2025 inayomalizika.

Mjumbe wa Kamati ya Ufundi ya Mtandao wa Wanawake, Katiba na Uchaguzi, Maria Chale, anasema wanatamani kuwa na Tanzania yenye ulinzi wa makundi ya wanyonge hasa wenye ulemavu na wanaoishi na ualbino.

Wanatamani ije dira inayoweka utaratibu wa kuwa na sheria ya kuwaadhibu kwa kunyongwa hadharani wanaoua wenye ualbino kwa sababu hayo ni mauaji ya kukusudia na wanaopatikana na hatia hawanyongwi mbali na kuhukumiwa na kubakia magerezani.

Maria anashauri sheria iangalie masuala ya ushahidi kwenye kesi za mauaji ya albino, badala ya kuendelea kueleza kuwa kesi ya mauaji ni lazima jamhuri itoe ushihidi usioacha shaka dhidi ya mshukiwa wa mauaji.



Dk. Amina Msengwa kutoka Tume ya Mipango na Uratibu wa Dira 2050, akizungumza wakati wa kupokea maoni ya wanawake. **PICHA ZOTE: MWANDISHI WETU**

Aidha, anazungumzia uendeshaji kesi za mauaji ya albino kuchelewa kupindukia akisema kuwe na utaratibu wa kuziharakisha zimalizike mahakamani na haki itendeke.

Mkurugenzi wa Taasisi ya Vivian Women, Vivian Ugulumu, anasema shirika lao linatamani kuona dira 2050 inayoifikisha Tanzania kwenye elimu bora na yenye wataalamu na wahandisi wa kutosha wazawa.

"Watoto wanasoma tena kwa kugharamiwa na serikali msingi na sekondari lakini wanapata elimu bora au bora elimu? Tufanye mabadiliko tuwe na elimu bora kama mataifa mengine Afrika Mashariki ikifika 2050 tuwe bora kielimu." Anasema.

Akizungumzia wahandisi anasema miaka ijayo ni lazima kuwa na wataalamu wazawa wanaojenga barabara za juu, za mwendokasi na kufanya kandarasi mbalimbali badala ya kutegemea wageni kama ilivyo sasa.

Katibu wa Chama cha Wasioona (TLB), Wilaya ya Kisarawe, Asha Magendo, anasema wanatamani kuona Tanzania inayoongozwa na dira inayoheshimu wanaoishi na ulemavu.

Anasema miaka 60 ya uhuru hakujawa na juhudi za kutosha kuwathamini na kuwaheshimu, mfano kwenye hospitali hakuna dirisha wala dawati kwa ajili yao.

"Usafiri wa umma hakuna anayewajali, ajira, wakiwa benki na vyoo vya umma au kwenye hoteli na migahawa hakuna anayetujali," anasema akitaka dira inayokuja iwe na Tanzania inayoheshimu wanaoishi na ulemavu.

Nice John ni Mjumbe wa Chama cha Wanaoishi na Ualbino (TAS) Wilaya ya Ilala, anasema dira inayokuja isisahau huduma muhimu kwa wanaoishi na ualbino kutokana na mabadiliko ya tabianchi.

"Dira inapoangalia makundi maalumu ihakikishe wenye ualbino wanapewa kofia, mafuta, miwani na tiba ya ngozi kutokana na jua kali na joto kutokana na mabadiliko ya tabianchi."

Vifaa hivyo vipatikana kwa kila mmoja anayehitaji kupitia Bohari ya Dawa (MSD) na sensa yao ifanyike iwatambue na kuwahudumia kwenye hospitali zote.

Nice anapendekeza kuwapo na madaktari bingwa wa ngozi na macho kwenye vituo vya afya mijini na vijijini ili kusaidia wanaoishi na ualbino.

"Tunatamani kuwa na dira inayozungumzia kuelimisha jamii kuhusu uelewa wa masuala ya ulemavu. Watu wafahamu sababu za ulemavu wowote na kuwaunga mkono kwa kukataa unyanyapaa," anaongeza Nice.

JUKWAA LA VIONGOZI

# Kagame Rais tena Rwanda ajizolea asilimia 99.15

• Aendeleza jambo lake kwa wapinzani




Paul Kagame, Rais wa Rwanda anayemaliza muda wake, akipiga kura Jumatatu wiki hii. **PICHA: AFP**

**Na Mwandishi Wetu**

WIKI ilipoanza Jumatatu Julai 15 ni siku ya kupiga kura nchini Rwanda, kumpata rais na wabunge.

Anayetetea kiti cha ikulu ni Rais Paul Kagame, aliyeishi madarakani tangu 2000 na sasa anawania muhula wa nne wa miaka mitano mingine.

Lakini, hayuko peke yake ana wapinzani wawili pekee ambao kwa mujibu wa vyombo vya habari ndiyo walioruhusiwa kuchuana naye. Japo inavyoelekea ni kama kiini macho.

Duru za kisiasa zinaeleza kuwa Rais Kagame na mgombea wa Chama cha Rwanda Patriotic Front (RPF), hadi jana asubuhi alikuwa amejihakikishia kubaki ikulu, akiongoza kwa asilimia 99.15 ya kura zilizopigwa.

Matokeo rasmi ya awali yakijumuisha asilimia 79 ya kura zilizohesabiwa Jumatatu usiku na Tume ya Taifa ya Uchaguzi (NEC).

Kwa mujibu wa matokeo haya yanayosomwa kwenye televisheni ya taifa na Mwenyekiti wa NEC, Oda Gasinzigwa, "mgombea wa chama cha Rwandan Patriotic Front, amepata asilimia 99.15 ya kura katika uchaguzi wa urais."

Aidha, anaendelea kueleza kuwa mpinzani wake mgombea wa chama cha Green Democratic Party, Frank Habineza, amepata asilimia 0.53 na mgombea binafsi Philippe Mpayimana ameshuka zaidi akipata asilimia 0.32.

Baada ya kutangazwa kwa matokeo hayo Jumatatu saa 4: 00, Kagame anazungumza moja kwa moja kutoka makao makuu ya chama chake cha RPF mbele ya wafuasi wake akiwaambia.

"Najua sio kila mtu yuko hapa usiku wa leo, lakini nilitaka kuwashukuru wote mmoja baada ya mwingine, kwa kuwa upande wangu hadi dakika ya mwisho, hatua hili ilipoamuliwa. Matokeo haya yako wazi, hakuna shaka tena sasa. Umewahi kuniona nikipoteza matumaini? Bila shaka hapana."

> "Najua sio kila mtu yuko hapa usiku wa leo, lakini nilitaka kuwashukuru wote mmoja baada ya mwingine, kwa kuwa upande wangu hadi dakika ya mwisho, hatua hili ilipoamuliwa. Matokeo

Anaongeza. "Iwe zamani ... au hata katika siku zijazo. Ni kwa sababu najua nina msaada wako na kwamba tutapata suluhisho pamoja kila wakati. Kuhusu asilimia hizi 99, ni za kuvutia sana. Na hata kama ningechaguliwa kwa asilimia 100... sio suala la idadi tu, ni taswira ya imani uliyonayo kwangu. Na hilo ndilo jambo muhimu zaidi kwangu. "

Kagame kwenye uchaguzi huo, anapambana na wapinzani 'walaini wale aliokutana nao uchaguzi uliopita wa urais mwaka 2017. Kiongozi wa chama pekee cha upinzani kilichoidhinishwa Frank Habineza na Philippe Mpayimana mgombea binafsi.

Wawili hao wanapambana dhidi ya Rais ambaye tayari amepata asilimia 98.79 ya kura kabla ya matokeo kamili yanatarajiwa kujulikana Jumamosi wiki hii Julai 20, kabla ya matokeo ya mwisho kutangazwa tena Julai 27.

Ripoti zinasema kuwa katika ofisi moja mjini Kigali, ambayo ilishuhudia kazi ya kuhesabu kura ni jina moja pekee lililosikika wakati wa kuhesabu kura la Paul Kagame, Rais anayemaliza muda wake kwa mara nyingine anawabwaga wapinzani wake.

Hapo awali, viongozi wakuu wa upinzani, ambao ni sauti muhimu zaidi katika uchaguzi na mstakabali wa demokrasi, waliondolewa kwenye kinyang'anyiro kabla ya uchaguzi.

**MSHINDI ALIFAHAMIKA**

Kwa mujibu wa vyombo vya habari, matokeo yake ni kama tayari yalikuwa yanajulikana. Na kwamba hakuna anayemuweza.

Hata hivyo, waliokwenda kupiga kura kwa kujivuna Jumatatu ilipofika wanamfahamu kiongozi mmoja pekee mkuu wa nchi yao.

Mpigakura mmoja anasikika akisema: "Nilikuwa na shauku kubwa ya kushiriki katika uchaguzi. Ndiyo maana nimeamka asubuhi sana. Shughuli ilikwenda vizuri sana, kulikuwa na ushiriki mkubwa. Na matokeo yake, ni kana kwamba ilikuwa tayari inajulikana, kwa kuwa tunajua vizuri kile tunachotaka. "

Wakati wa kampeni yake, Rais Kagame kila mara alisimama na kuonekana kujiamini, akiwasilisha uchaguzi huu mpya kama utaratibu. Ujumbe uliopokelewa vyema na wapigakura.

Baada ya mageuzi ya katiba yaliyopitishwa mwaka 2015, Paul Kagame, bado anaweza kuiongoza Rwanda kwa mihula miwili ya miaka mitano, hadi 2034.

**KUBANA WAPINZANI**

Kagame anafahamika kwa kubinya wapinzani na kwa sasa kiongozi wa upinzani Victoire Ingabire , alikatazwa kuwania kiti cha urais kwenye uchaguzi wa mwaka huu baada ya mahakama ya juu nchini humo kumzuia kugombea.

Majaji wa Mahakama ya Juu mjini Kigali walitupilia mbali ombi la Victoire Ingabire la kutaka kurejeshewa haki yake ya uraia wa Rwanda na hivyo kumzuia kugombea katika uchaguzi wa urais.

Kiongozi huyo wa upinzani anaviambia vyombo vya habari kwamba hata hivyo aliheshimu masharti yote yaliyowekwa baada ya yeye kuachiliwa huru kwa msamaha wa rais mwaka 2018.

Anasema uamuzi huu wa mahakama si jambo la kushangaza kwa sababu serikali ya Kagame haitaki upinzani unaoaminika.

"Chama tawala, RPF, hakiko tayari kuwapa nafasi wapinzani, hakiko tayari kushindana na wengine ambao wana sera ambayo Wanyarwanda wanaweza kupata fursa ya kuchagua."Anaongeza.

Anasema chama cha RPF hakiko tayari kukubali ushindani. Lakini wakati huo huo, Wanyarwanda wana kiu ya demokrasia, wana hamu ya kuwa na nchi ambayo inaweza kujieleza kwa uhuru.

Victoire Ingabire alikamatwa na kutuhumiwa kukana ukweli wa mauaji ya halaiki nchini Rwanda, baada ya kuomba mnamo mwaka 2010 kwamba wahusika wa uhalifu dhidi ya Wahutu pia wahukumiwe.

***DW /RFI***



HABARI DODOMA

# Kaya 300 zaaga umaskini kwa miradi

**Na Peter Mkwavila,** CHAMWINO

SHIRIKA la Brac Maendeleo Tanzania limefadhili kaya 300 wilayani hapa Mkoa wa Dodoma katika miradi ya ufugaji na mitaji ya fedha za kuanzisha biashara.

Mratibu Miradi wa Brac wilayani hapa, James Komba alibainisha hayo jana wakati akizungumza na viongozi wa serikali akiwa kwenye ziara ya kukagua miradi wanayofadhili.

Komba, alisema kaya hizo zimewawezesha pia kupata uelewa wa kutunza na kutumia fedha zao kwa malengo yaliyokusudiwa kulingana na mahitaji yao.

Alisema kwa Chamwino wamezifikia kaya 519, kati ya hizo 300 zimefadhiliwa kwa kupatiwa miradi na fedha.

"Tumevifikia vijiji vinne vya Mvula, Muungano Majereko na Chinangali ambako tumekutana na kaya maskini," alisema Komba.

Mmoja wa wanufaika, Melea Obed, Mkazi wa Kijiji cha Majeleko, alisema ameondokana na umasikini, utegemezi na tabia ya kuombaomba mitaani kutokana na ulemavu baada ya kiasi cha mtaji alichopewa kumuwezesha kufungua duka.

"Miradi hii imetuwezesha hata kuwasomesha watoto shule, kubuni miradi mingine kupitia kipato tunachokipata na tumeajiri watu wengine kupitia mpango huu wa Brac Maendeleo Tanzania," alisema.

Monica Hamanda, alisema mradi wa ufugaji wa mbuzi umesaidia kuongeza uelewa wa kazi hiyo na biashara.

Shirika hilo limeziwezesha kaya hizo kuanzisha miradi mingine ya ufugaji ng'ombe, nguruwe, kondoo, kuku na bata.

**"Tumevifikia vijiji vinne vya Mvula, Muungano Majereko na Chinangali ambako tumekutana na kaya maskini," alisema Komba.**

# Duka la dawa lafungwa kwa kufanyia upasuaji wagonjwa

**Na Thobias Mwanakatwe,** ITIGI

HALMASHAURI ya Wilaya ya Itigi mkoani Singida imelifungia kutoa huduma duka la dawa muhimu lililopo Kitongoji cha Kashamawele kwa kukiuka sheria na kufanya upasuaji kwa wagonjwa.

Imebainika kuwa duka hilo, pia lilikuwa linaendeshwa bila kusajiliwa na kuuza dawa ambazo muda wake wa matumizi umekwisha

Duka hilo lilibainika juzi baada ya timu ya wataalamu wa afya wakiongozwa na Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo, Dk. Emmanuel Mallange na kukuta likitoa huduma kinyume cha sheria

Mmiliki wa duka hilo jina lake halikupatikana kutokana na kukimbia na kutokomea kusikojulikana kwa kuhofia kukamatwa baada ya kupata taarifa za ujio wa wakaguzi hao wa afya kutoka halmashauri hiyo.

Dk. Mallange, alisema baada ya kufanya ukaguzi, walikuta dawa ambazo hazitakiwi kuuzwa dukani ikiwa ni pamoja na za usingizi na zilizokwisha muda wa matumizi.

Alisema inadaiwa kuwa mmiliki wa duka hilo amekuwa akijitambulisha kwa wananchi kuwa yeye ni daktari na amekuwa akitoa huduma mbalimbali ikiwamo upasuaji mdogo na kulaza wagonjwa.

Aliuagiza uongozi wa Kitongoji cha Kashamawele kumsaka na kumkamata mmiliki huyo na kumfikisha Ofisi ya Mganga Mkuu wa Halmashauri hiyo ili hatua za kisheria zichukuliwe dhidi yake

Vilevile, aliwataka wananchi kuacha kwenda kupata huduma katika duka hilo kwa kuwa ni hatari kwa afya zao.

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya, kutumia dawa iliyokwisha nguvu na usalama ni hatari kwa afya kwani inaweza kuleta madhara kama usugu wa vimelea vya magonjwa na kifo.

Dawa zinazotolewa kwa njia ya sindano pia si salama kuzitumia baada ya kwisha muda kwani zinaweza kusababisha madhara makubwa kutokana na vijidudu kuota kwenye dawa hizo zenye asili ya majimaji au unga na kuleta madhara makubwa zaidi endapo wataingia mwilini



Msimamizi wa mradi wa kuwezesha kaya maskini kutoka shirika lisilo la kiserikali la Brac- Maendeleo Tanzania ikiwemo watu wenye ulemavu, Latifa Saninga akimsaidia kusukuma baiskeli, Melea Obedi ambaye ni mjasiriamali mwenye ulemavu wa viungo wa Kijiji cha Majereko Wilaya ya Chamwino mkoani Dodoma baada ya kutembelewa na maofisa wa shirika hilo jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Jafo ashtushwa Watanzania wachache kutumia mbolea

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Viwanda na Biashara, Dk. Selemani Jafo ameonyesha kushtushwa na idadi ndogo ya Watanzania kutumia mbolea inayozalishwa katika kiwanda cha ndani cha Intracom.

Akizungumza kwenye ziara ya kukagua uzalishaji wa mbolea kwenye kiwanda hicho jijini hapa ambacho ni matunda ya ziara ya Rais Samia Suluhu Hassan alipokuwa nchini Burundi, alisema kina uwezo wa kuzalisha tani milioni moja kwa mwaka.

Jafo, alisema kati ya kiwango kilichozalishwa kwa sasa takwimu zinaonyesha kiasi kidogo kimeuzwa nchini.

"Kwenye taarifa nimeona kuna uzalishaji uliofanyika wa tani 76,000 na kati ya hizo 60,000 ziliuzwa na zilizouzwa nchini pekee ni 4,000, sijafurahishwa na hali hii kama Rais amehangaika hadi kuleta kiwanda hiki nchini, mimi nikiwa Waziri wa Viwanda sitakubali hata kidogo juhudi zake zipotee," alisema Jafo na kuongeza kuwa:

"Sijafurahishwa na mwenendo huu, tunafanya uwekezaji mkubwa katika sekta ya kilimo Rais ameongeza bajeti ya kilimo kutoka Sh. bilioni 294 hadi Sh. trilioni 1.2 ni wazi ana matamanio makubwa sana, niwaombe Watanzania kutumia mbolea ya kiwanda hiki," alisema.

Alisema kiwanda hicho uwekezaji wake ni zaidi ya Sh. bilioni 500 na ujenzi bado unaendelea maeneo mengine na inatarajiwa uwekezaji uwe zaidi ya Shilingi trilioni moja.

"Kiwanda kina waajiriwa 907 na zaidi ya 600 ni Watanzania na kitakapokamilika uwezo wake ni kuajiri watu 3,000 hadi 4,000, haiwezekani mbolea izalishwe hapa isinunuliwe Tanzania hii ni kumkwamisha Rais, kwanini tununue mbolea maeneo mengine nje ya nchi lakini tushindwe kununua hapa nchini."

"Mimi Waziri wa Viwanda sitakubali hata kidogo kuona viwanda vinavyojengwa Tanzania vinashindwa kuwezeshwa kufanya kazi yake hii kubwa, sisi kama serikali tutajadiliana namna ya kufanya ili viwanda vinavyojengwa nchini vifanye kazi vizuri," alisema Waziri huyo ambaye pia ni Mbunge wa Kisarawe.

Aliwahakikishia wawekezaji kuwa atahakikisha viwanda vilivyowekezwa nchini vinakidhi matarajio ya Rais Samia.

"Tutavilinda viwanda vyetu hapa nchini vifanye kazi vizuri na vijana wetu wapate ajira na dhamira ya Rais Samia ya kuhangaika kutafuta wawekezaji lazima itimie," alisema.

Mkurugenzi wa Kiufundi wa Kiwanda hicho, Victor Ngendazi, alisema kilianza kujengwa Julai mwaka 2021 kwa lengo la kutengeneza tani 600,000 za mbolea na kwamba kutokana na maombi ya serikali wameongeza hadi kufikia tani milioni moja.

"Kwa sasa ujenzi unaendelea kwenye maeneo yaliyosalia, tunataka eneo hili tuwe na viwanda vitano na tayari vitatu vinafanya kazi na uzalishaji kwa ujumla utaanza Agosti, mwaka huu baada ya kukamilisha majaribio ya mitambo ya viwanda viwili," alisema Ngendazi.

Alisema wamekuwa wakishirikiana na serikali kutatua changamoto zilizokuwa zikiwakabili.





# 'Watanzania changamkieni fursa za kilimo ndani, nje'

**Na Gwamaka Alipipi**

WATANZANIA wamehimizwa kuchangamkia fursa mbalimbali zinazojitokeza katika sekta ya kilimo ndani na nje ya nchi.

Wito huo umetolewa na Mkurugenzi Mtendaji wa Kilimo Roundtable, Rhoda Mwita wakati akizungumza na waandishi wa habari akisema kuna mustakabali mzuri kwa vijana wa kitanzania katika kilimo na mamilioni ya fursa za kuchangamkia.

Alisema dhamira ya jukwaa hilo ni kukuza sekta ya kilimo kuwa endelevu na yenye mafanikio Tanzania na Afrika.

"Sasa ni wakati wa Watanzania kuutumia uwezo mkubwa uliopo katika sekta yetu ya kilimo," alisema Rhoda huku akielezea miaka 24 ya uzoefu wake katika kusaidia wakulima kuboresha afya ya udongo.

Kadhalika alisema: "Kuna mustakabali mzuri kwa vijana wa kitanzania katika kilimo, mamilioni ya fursa za kuchangamkia. Kwa msaada unaofaa na ubunifu, wakulima wetu na biashara za kilimo zinaweza kuwa mstari wa mbele katika kubadilisha uchumi wetu na kuhakikisha usalama wa chakula na uendelevu kwa kanda nzima."

Pia, aliisifu Wizara ya Kilimo kwa agenda ya uwekezaji 10/30 ya kuharakisha ukuaji wa kilimo nchini.

Alisema wanakusudia kuongeza mauzo ya nje ya mazao ya kilimo na kuunda fursa mpya kwa mazao ya thamani ya juu ambayo yanaweza kuwafaidisha wakulima, wafanyabiashara na taifa.

Akizungumzia kuhusu mkutano wa kwanza wa wadau wa kilimo utakaofanyika Dodoma wakati wa maadhimisho ya Nane Nane, alisema: "Ni gala ya kwanza kwa mwaka huu, itakayohamasisha ushirikiano, ubunifu, na ukuaji ili kuisukuma Tanzania kulisha Afrika na ulimwengu, inalenga kuitangaza sekta ya kilimo ya Tanzania kimataifa na kukuza ukuaji endelevu."

Alisema gala hiyo itahusisha wadau wote katika mnyororo wa thamani wa kilimo, wakiwemo wakulima, biashara za kilimo, watunga sera, wawekezaji na wabunifu ili kuja pamoja na kushirikiana.



Mamalishe na babalishe wa Soko la Sido jijini Mbeya, wakipiga makofi kama ishara ya kumkaribisha Katibu Tawala wa Wilaya ya Mbeya, Mohamed Aziz (hayupo pichani) mwishoni mwa wiki iliyopita alipokuwa mgeni rasmi kwenye uzinduzi wa karo la kuoshea vyombo ambalo limejengwa sokoni hapo ikiwa ni sehemu ya miradi ya ushirikiano kati ya Jiji la Mbeya na Jiji la Zurich la nchini Uswis. **PICHA: NEBART MSOKWA**

## W' biashara Mazimbu wamuomba Samia maeneo

**Na Christina Haule,** MOROGORO

WAFANYABIASHARA wadogo wa Soko la Mazimbu Road Manispaa ya Morogoro wamemuomba Rais Samia Suluhu Hassan kuwajengea maeneo ya kudumu ya kufanya biashara.

Wamesema wanahitaji maeneo mazuri kama ilivyo eneo la Feri -Mvomero na Mtumbatu -Gairo ili kuhudumia jamii na wasafiri wa nchi jirani wanaopita kwenye eneo hilo.

Akizungumza na waandishi wa habari, Mwenyekiti wa soko hilo lenye wafanyabiashara zaidi ya 150 waliokaa kwa zaidi ya miaka 15 mahali hapo, Khaji Hassan alisema hawapingi kuondoka kwenye eneo hilo kwa ajili ya kupisha upanuzi wa barabara kwa sababu wanafahamu sheria haiwaruhusu kubaki hapo.

Alisema wamestushwa na tangazo la ghafla lililotolewa Julai Mosi mwaka huu likiwataka kuwa wameshaondoka hadi ifikapo Julai 7, kwamba hawajui hatima yao watakwenda wapi.

Hassan alisema wakiwa wafanyabiashara wa mali mbichi ikiwemo nyanya, embe, mananasi, machungwa, ndizi za kuiva, samaki na vingine wanashindwa kuondoka kutokana na kutopata mahali sahihi na rafiki kwa kuuza biashara zao.

Alisema baada ya tangazo hilo walilazimika kuandamana hadi ofisi ya Wakala wa Barabara Tanzania (TANROADS) mkoani Morogoro, ili kujiridhisha ukweli wa tangazo hilo.

Alisema TANROADS waliwahakikishia kuwa kweli wanapaswa kuhama kwa mujibu sheria ili kupisha upanuzi wa Barabara ya Morogoro-Dodoma.

Alisema wakalazimika kwenda kwa Mkuu wa Wilaya Morogoro, Rebecca Nsemwa ambaye naye aliwahimiza kuhama kwa madai kuwa tayari wameshapewa maeneo ambayo hata wao hawayajui.

Hassan alisema wamefanya biashara ene hilo kwa miaka mingi, huku wengine wakiwa na mikopo kutoka taasisi za kifedha.

Baadhi ya wafanyabishara wa eneo hilo, Getruda Kamnge aliiomba serikali iwafikirie sababu eneo walilopo ni Katikati na wanawauzia wapita njia wakiwemo wanaokwenda Burundi, Uganda na Zimbabwe.

Naye Nicola Ngatunga ambaye aliiomba serikali kuwapa muda wa kuhama hata miezi mitatu, ili waweze kujipanga na kutafuta sehemu ya kwenda na wasiharibu biashara zao.

## Sita wafariki dunia kwa kuvuta hewa ya mkaa

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WATU sita mkoani Njombe wamefariki dunia kwa kuvuta hewa ya mkaa wakati wakiota moto nyumbani.

Hayo yalielezwa na Kamanda wa Polisi Mkoa wa Njombe, Kamishna Msaidizi Mahamoud Banga, wakati akizungumza na waandishi wa habari ofisini kwake.

Alisema vifo hivyo ni vile vilivyoripotiwa kwa Jeshi la Polisi kwa kipindi cha miaka minne.

Kamanda Banga alitahadharisha wananchi dhidi ya matumizi ya mkaa hasa majira ya usiku akisema unaweza kusababisha madhara ya kiafya hadi vifo.

"Kwa hiyo tunaendelea kutoa wito kwa wananchi mkoani Njombe kwamba wakati huu ni wakati wa baridi na wakati wa baridi wananchi wamekuwa wakitumia sana majiko haya ya mkaa ambayo yana sumu," alisema Banga.

Kwa upande wa wakazi wa Njombe akiwemo Maria Sanga alisema kutokana na hali ya baridi inawalazimu kuota moto lakini pia wanachukua tahadhari.

# Wapewa siku saba kuhamia Soko la Kiumba

**Na Elizabeth John,** NJOMBE

WAFANYABIASHARA wa mazao katika Halmashauri ya Mji wa Makambako wilayani Njombe wamepewa siku saba kuhamia Soko la Mazao Kiumba.

Pia, magari yanayobeba viazi yakitakiwa kushusha Soko la Magegele, magari mali mbichi husuani matunda yakitakiwa kushusha Soko la Maguvani.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Kenneth Haule alitoa agizo hilo juzi wakati akizungumza na wafanyabiashara wa mazao katika ofisi za halmashauri hiyo.

Alisema hatua hiyo ni kufuatia agizo lililotolewa na Mkuu wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka la kuwataka wafanyabiashara 112 ambao waliingia ubia na halmashauri kujenga Soko la Mazao Kiumba kuhamia katika soko hilo bila kuwaathiri wale wenye mitaji midogo.

Pia, aliiagiza halmashauri kuzuia magari kushusha na kupakia mazaokatika Soko Kuu la Makambako.

Haule alisema magari makubwa ambayo yanabeba viazi yatalazimika kwenda kushusha Soko la Magegele na ya mali mbichi kushusha Soko la Maguvani na mazao yote Soko la Kiumba, huku akiwataka wafanyabiashara wadogo kuendelea kufanya biashara katika masoko waliyopo.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Hanana Mfikwa alisema baada ya wiki moja kupita zoezi la kuzuia magari kutoshusha mazao katika soko kuu litaanza na kwa wale watakaokiuka watapigwa faini ambayo ni kuanzia Sh. 200,000 hadi milioni moja.

Naye Ofisa Biashara wa Halmashauri ya Mji wa Makambako, Caros Mhenga alisema zoezi hilo litasaidia kuupanga mji na kutanua wigo wa biashara kwa wananchi na kueleza kuwa watasimamia vema ili kuhakikisha zoezi hilo linafanikiwa bila kuleta adha kwa wafanyabiashara.



HABARI ZANZIBAR

# Makamu wa Rais ataja faida viwanja vya ndege

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdulla amesema viwanja vya ndege ni sehemu muhimu kwa ukuaji wa uchumi wa Zanzibar, inategemea zaidi shughuli za utalii ambazo zinakwenda sambamba na uwepo wa miundombinu mizuri ya viwanja hivyo.

Aliyasema hayo jana visiwani Zanzibar alipofanya ziara ya kutembelea na kukagua maendeleo ya ujenzi wa miradi mbalimbali inayojengwa na Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar.

Hemed alisema viwanja vya ndege ni milango mikuu ya nchi yoyote duniani inayotumika kwa kusafirishia wageni ambao huchangia kwa kiwango kikubwa kukua kwa uchumi na kuongezeka kwa pato la nchi husika.

Alisema utakapokamilika ujenzi wa miradi ya viwanja vya ndege vya jengo la kwanza na la pilli la abiria na eneo la biashara itaondoa changamoto ya msongamano wa abiria wanaokaa muda mrefu kusubiri kuhudumiwa.

Alisema pia itaongeza uwezo wa kutoa huduma bora na za haraka jambo ambalo litapelekea wageni wengi kuendelea kuitembelea Zanzibar mara kwa mara.

Hivyo, alimtaka Mkurugenzi wa Mamlaka ya Viwanja vya Ndege Zanzibar kuhakikisha kila penye uwezekano wa kupatikana kwa kodi kuhakikisha kodi hiyo inakusanywa na kuingia serikalini ili kuendelea kuimarisha na kuboresha huduma za kijamii kwa wananchi wa Zanzibar.

Aidha, alisema serikali itaendelea kutoa ushirikano kwa kampuni zote zinazojenga miradi nchini ikiwemo kampuni ya Estim Constraction inayojenga miradi ya viwanja vya ndege vya Zanzibar, ili kuhakikisha wanakabidhi miradi hiyo kwa wakati uliopangwa na kwa kuzingatia viwango na ubora. Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji, Dk. Khalid Salum Muhammed alisema uchumi wa Zanzibar unategemea zaidi utalii, hivyo ni lazima kuimarisha miundombinu ya kimkakati ikiwemo viwanja vya ndege ili kuhakikisha utalii unakuwa kwa kasi zaidi na pato la nchi linaongezeka kupitia wageni wanaoingia Zanzibar.

Alisema ujenzi wa miradi hiyo inaendelea vizuri na hakuna changamoto yoyote hadi sasa ambayo itasababisha kuchelewa kukamilika kwa ujenzi wa miradi hiyo.

Aliahidi kuwa uongozi wa wizara utahakikisha miradi yote inakamilika kwa wakati na kwa kiwango kilichokusidiwa ili kufikia malengo ya serikali iliyojiwekea.

Mshauri elekezi kutoka kampuni ya Anova Consult, Ibrahim Gasper alisema hadi sasa miradi yote inakwenda vizuri na ipo ndani ya wakati. Hivyo, alimhakikishia Makamu wa Pili wa Rais kuwa watakabidhi miradi hiyo ndani ya muda uliopangwa na kwa kuzingatia viwango vya hali juu.



Baadhi ya wananchi wakiwa katika fukwe ya Bahari ya Kijiji cha Pwani Mchangani mjini Zanzibar wakinunua madafu. Dafu moja huuzwa kwa Sh. 1000. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Mwinyi kufungua maonesho Nanenane

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WIZARA ya Kilimo, Maliasili, Umwagiliaji na Mifugo imesema serikali imeazimia kufanya maonyesho ya kilimo kila ifikapo Agosti 8 ya kila mwaka, kwa kutambua umuhimu wa sekta ya kilimo nchini kama uti wa mgongo wa uchumi wa nchi.

Akizungumza jana na waandishi wa habari visiwani Zanzibar kuhusu maandalizi ya maonyesho hayo, Waziri wa Wizara hiyo, Shamata Shaame Khamis alisema kwa mwaka huu serikali itafungua rasmi maonesho hayo Agosti tatu katika viwanja vya maonesho Kizimbani.

Alisema maonyesho hayo yatakayodumu kwa siku 14 ambayo yatafunguliwa na Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi.

Waziri Shamata alisema wizara yake imekamilisha matayarisho na ina lengo la kufanya mageuzi ili kukibadilisha kilimo kilichozoeleka na kuwa himilivu na chenye tija.

Alisema mageuzi hayo ni muhimu, yanatarajia kuimarisha mnyonyoro wa thamani kutoka shambani hadi kufika kwa mlaji, ambapo kila mtu atakayeshiriki katika mnyororo huo atafaidika na matunda ya mageuzi hayo.

"Sekta hii ya kilimo inaunganisha sekta nyingi muhimu ikiwemo biashara, viwanda, utalii, maji na nishati. Hivyo, sekta ya kilimo ikifanya vizuri itasababisha kuleta matokeo chanya kwa uchumi wa nchi yetu. Kupita juhudi hizo kila mdau anatakiwa kushiriki kikamilifu na kuunga mkono azma ya kuleta mageuzi haya" alisema.

Aidha, alisema anaamini kwamba kupitia maonesho hayo kutakuwa na ongezeko la washiriki na wananchi watakaotembelea.

Alisema kuwa hivi sasa zao la nazi limehadimika kutokana na minazi kukatwa kwa sababu mbalimbali ikiwemo ujenzi.

Alisema serikali kupitia wizara hiyo imeshaanza kuweka mikakati ya kutatua changamoto hiyo ili zao hilo kurudi kama zamani na Zanzibar kusifika kwa uzalishaji.

# Waziri ataja mbinu kuokoa uharibifu mazingira

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WAZIRI wa Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Shaaban Ali Othman, amesema ili kutatua changamoto za wavuvi na uharibifu wa mazingira ya baharini, lazima kuwepo ushirikiano wa pamoja kati ya viongozi wa mikoa, wilaya na masheha.

Alisema kumekuwa na uharibifu mkubwa unaofanyika katika maeneo tengefu ya bahari sambamba na kukithiri kwa uvuvi haramu nchini.

Aliyasema hayo jana katika kikao kilichofanyika ofisi za Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja kujadili namna ya kutatua changamoto za wavuvi juu ya matumizi mabaya ya zana za uvuvi zisizokubalika kisheria.

Alisema serikali inatarajia kutoa boti kubwa zenye vifaa kamili kwa wavuvi wa Kijiji cha Chwaka ili waondokane na uvuvi waliozoea na kuvua kisasa, kwa lengo la kuimarisha uhifadhi wa bahari na rasilimali zake.

Aidha alisema lengo la kukutana na viongozi wa mkoa huo ni kufanya maamuzi ya pamoja kupitia maombi ya wavuvi wa Chwaka ambayo yataendana na masharti ya serikali.

"Ni vema wavuvi muwe tayari kukubaliana na maamuzi ya serikali kwa kuacha uchafuzi wa mazingira katika maeneo tengefu pamoja na uvuvi haramu unaorejesha nyuma juhudi zetu za kuimarisha ukuaji wa uchumi nchini," alisema.

Mkuu wa Mkoa wa Kusini Unguja, Ayoub Mohammed Mahmoud, alisema viongozi hao wanaunga mkono hatua ya Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi kuwapatia boti wavuvi wa Chwaka inayolenga kutatua changamoto zilizomo katika eneo lao.

Hivyo, aliwataka viongozi wa sekta nyingine kutoa ushirikiano wa pamoja ili kujenga imani za wananchi kwa ajili ya kuwaletea maendeleo kupitia uchumi wa bluu.

Mkuu wa Wilaya ya Kati Unguja, Sadifa Juma Khamis, aliwataka wavuvi kufuata utaratibu uliowekwa ili kuondoa migogoro inayojitokeza mara kwa mara kati yao na serikali.

Akizungumza katika kikao hicho, Mbunge wa Chwaka, Haji Makame Mlenge, aliitaka Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi kufanya haraka kukamilisha taratibu za kuwapatia wananchi mikopo nafuu ya boti ili waondokane na uvuvi katika maeneo tengefu ya bahari pamoja na matumizi ya zana zisizokubalika kisheria.


# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## KUPOTEA KWA CHETI



**GODLIVER ERASTO MTAHEBA,** Anatangaza kupotelewa na cheti cha chuo chenye namba ya usajili **IRDP/CRP/12/2493** kilichotolewa na chuo cha Mipango Mwaka 2013. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo cha Polisi. TAARIFA YA POLISI **KAS/RB/3035/2020**

## KUPOTEA KWA HATI YA KUSAFIRIA



**EVELINA NESTORY RUTAGELEKWA** Anatangaza kupotelewa na hati ya kusafiria yenye namba **TAE243854** iliyotolewa na Idara ya uhamiaji jijini Dar Es Salaam, mwaka 2019. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo jirani yake. Taarifa ya polisi. **PHQ/SHI/KAH/5289/2024.**

## KUPOTEA KWA CHETI



**DICKSON JAPHET KIWALE** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0768/0055** kilicholewa na **ST. BENEDICT SEKONDARI** Mwaka 2016. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MKO/RB/1218/2024.**

## KUPOTELEWA NYARAKA YA UMILIKI KIWANJA

**JOSEPH H MALALE**

anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki kiwanja namba **265 kitalu "j j"** kilichopo Ndembezi Manispaa ya Shinyanga.

Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu

Taarifa ya polisi

**PHQ/SHI/SHI/5149/2024**

## KUPOTEA KWA HATI MILIKI YA VIWANJA

**MUSSA JAFARI KIDELI**

Anatangaza kupotelewa na Hati miliki ya viwanja, vyenye namba **P11244, P11246.** Kwayeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake.

**PHQ/MOR/MOR/22106/2024**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**SADIKI BAKARI NGOMA**

anatangaza kupotelewa na kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **T 981 BLX** aina ya FEKON. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote che polisi.

Taarifa ya polisi:

**PHQ/TAN/HAN/7188/2024**

## KUPOTELEWA NYARAKA UMILIKI KIWANJA

**MADOLI SEYENGO**

anatangaza kupotelewa na nyaraka ya umiliki kiwanja namba **674 kitalu "CC"** kilichopo Matanda Manispaa ya Shinyanga

kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilichopo karibu

Taarifa ya polisi

**SHI/SHI/RB/417079/2022**

## KUPOTEA KWA HATI YA NYUMBA

**YUSRIA SAAD MBAROUK**

anatangaza kupotea kwa hati ya nyumba yenye **PLOT NO. 528 BLOCK 'E' iliyopo SINZA** wilaya ya KINONDONI mkoa wa DAR ES SALAAM. Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi.

POLISI TAARIFA:

**PHQ/DAR/UBU/145553/2024**

---

**IN THE HIGH COURT OF THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MOSHI SUB- REGISTRY**
**AT MOSHI**
**MISC.LAND APPLICATION NO.2800 OF 2024**

**(C/F Applicatio NO. 14 of 2020 in the Moshi District Land and Housing Tribunal in Application)**

**ALPHA JOSEPH KAAYA.................... ...............APPLICANT**

**VERSUS**

**FESTO SAMSON MOSHI..........................................1st RESPONDENT**
**ELIZABETH SAMSON MOSHI.................................2nd RESPONDENT**
**JOSEPH MLINGI.....................................................3rd RESPONDENT**
**FRANK MASSAE.....................................................4th RESPONDENT**
**WILSON MLANGA MUSHI.......................................5th RESPONDENT**
**TO: FRANK MASSAE.**

**NOTICE FOR MENTION,**

**TAKE NOTICE** that the above case has been fixed for mention in the High Court of Tanzania at Moshi on 6th day of August, 2024 at 9:00 a.m. before **Honourable L. M. MONGELLA, judge.**

**WHEREAS:** Service on you has been ordered to be published in the Nipashe Newspaper .

You may appear in person or by Advocate or agent dully authorized to appear on your behalf and you are directed to produce on that day all the documents upon which you intend to rely upon in support of your case.

**TAKE FURTHER NORE THAT:** in default of your appearance on that day and time the court may proceed in your absence.

**GIVEN UNDER** my hand and seal of the Court this 03rd day July ,2024

DEPUTY REGISTRAR
DEPUTY REGISTRAR
HIGH COURT OF TANZANIA
MOSHI

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KINONDONI**
**AT KINONDONI**
**CIVIL CASE 25550 OF 2024**

**BANK OF AFRICA................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**BONIPHACE JACOB MBIRU.........DEFENDANT**

**TO: BONIPHACE JACOB MBIRU**

**NOTICE DATE FOR JUDGEMENT**

**THE NOTICE** that the above case has been fixed to mention on 25th day of JULY, 2024 at 08:30 a.m Before **Hon. JANETH KALUYENDA – PRM.**

**YOU ARE** required to appear in this Court without failing and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

Given under my Hand and the Seal of the Court this 15th day of July, 2024.

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF ILALA**
**AT KINYEREZI**
**CIVIL CASE 05 OF 2023**

**BANK OF AFRICA TANZANIA LTD............PLAINTIFF**

**VERSUS**

**JESSE RUTALEMWA RUMANYISHA..................DEFENDANT**

**NOTICE OF EX-PARTE JUDGEMENT**

**THE NOTICE** that the above case has been fixed for Ex-Parte Judgment on 19 day 07, 2024 at 10:00a.m Before **Hon. GLORY E. NKWERA – SRM, RM.**

**YOU ARE** required to appear in Court without fail in which Ex-parte Judgment will be delivered by the court.

Given under my Hand and the Seal of the Court this **16th day of 07, 2024.**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

---

**IN THE DISTRICT COURT OF KINONDONI**
**AT KINONDONI**
**CIVIL CASE 25550 OF 2024**

**BANK OF AFRICA................PLAINTIFF**

**VERSUS**

**LYDIA PETER...................DEFENDANT**

**TO: LYDIA PETER**

**NOTICE DATE FOR JUDGEMENT**

**THE NOTICE** that the above case has been fixed to mention on 25th day of JULY, 2024 at 08:30 a.m **Before Hon. JANETH KALUYENDA – PRM.**

**YOU ARE** required to appear in this Court without failing and you must produce on that day all the documents upon which you intend to rely in support of your case.

Given under my Hand and the Seal of the Court this **15th day of July, 2024.**

SENIOR RESIDENT MAGISTRATE

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**KUITWA SHAURINI**

**MADAI NO. 12783/24**

**MDAI: TATA AFRICA HOLDINGS (T) LTD**

**MDAIWA: GERMIN ENGINEERING CO. LTD**

Madai hayo yamefunguliwa katika mahakama hii ndugu Germin Engineering Co. Ltd

Unaamriwa na mahakama hii kuhudhuria mnamo tarehe 29/7/24 na usipohudhuria shauri litasikilizwa upande mmoja na uamuzi kutolewa.

RESIDENT MAGISTRATE
TEMEKE DISTRICT COURT

---

**IN THE RESIDENT MAGISTRATE'S COURT OF DAR ES SALAAM**
**AT KISUTU**

**CIVIL CASE NO...........OF................**

**AMIK TRANSPORT TANZANIA LIMITED...CLAIMANT**

**VERSUS**

**SIMBA LOGISTICS EQUIPMENT'S SUPPLY LIMITED....................................RESPONDENT**

**NOTICE OF DATE OF EXPARTE JUDGEMENT**

**TAKE NOTICE** that, the above mentioned case has been fixed for ex-parte Judgment on the **19 day of July, 2024 at 1:00 pm. Before Hon. RUBOROGA – PRM.**

Please be so informed

**GIVEN** under my hand and the **SEAL** of the Court this **10th day of July, 2024.**

PRINCIPAL RESIDENT MAGISTRATE

---

**OFISI ZA MATANGAZO**
**MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,**
**PO.BOX 31042,**
**DAR ES SALAAM.**
**MOB: +255 - 745 700 710.**
**E-mail:**
**advertise@guardian.co.tz,**
**website:**
**www.ippmedia.com**

---

KWA MAHITAJI YA KUTANGAZA SUMMONS, KUPOTEA KWA CHETI, KUPOTEA KWA KADI YA GARI/PIKIPIKI NA USIMAMIZI WA MIRATHI.

TUPIGIE: +255 - 0677 020701

AU

TEMBELEA OFISI ZA MATANGAZO
MIKOCHENI INDUSTIAL AREA,
PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM.
E-MAIL: ADVERTISE@GUARDIAN.CO.TZ

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

Kwa

HABARI KIMATAIFA

# Kagame ashinda kwa kishindo uchaguzi wa urais Rwanda

**KIGALI,** RWANDA

RAIS wa Rwanda, Paul Kagame, ameshinda muhula wa nne katika uchaguzi wa urais na bunge kwa kupata asilimia 99.15 ya kura milioni saba zilizohesabiwa hadi jana.

Ilielezwa kuwa wapigakura walioshiriki uchaguzi huo ni milioni tisa, ambako Frank Habineza wa Chama cha Green Party of Rwanda (DGPR) alipata asilimia 0.53 ya kura zilizokwisha hesabiwa huku mgombea binafsi Phillipe Mpayimana akipata asilimia 0.32.

Baada ya kutangazwa matokeo hayo, Rais Kagame aliwapongeza wananchi wote walioshiriki zoezi la uchaguzi lakini pia akawapongeza kwa namna ya kipekee wakuu wa vyama vya siasa vilivyofanya mseto na chama tawala cha RPF.

"Ushindi wa matokeo haya mnaouona ni muungano wa wafuasi wa wanachama wetu wa RPF vyama vingine washirika wetu," alisema Kagame akiwanyooshea mkono wa shukrani viongozi hao waliokuwa wamesimama nyuma yake.

Kiongozi wa Chama cha Green Party of Rwanda, Frank Habineza, alimpongeza Rais Kagame kwa ushindi huo huku Pillipe Mpayimana mgombea binafsi akisema hata kama hesabu zinaonyesha ameshindwa lakini bado ana imani kwamba atafanya vizuri siku za usoni na kwamba kikubwa kwake alionyesha uzalendo wake kwa kugombea nafasi ya urais.

Ilielezwa kuwa zaidi ya watu milioni tisa walijiandikisha katika daftari la wapigakura huku milioni mbili kati ya hao wakipiga kura kwa mara yao ya kwanza wengi wao wakiwa ni vijana wa chini ya miaka 20.

Pia ilielezwa kuwa matokeo hayo yanakamilisha mchakato wa kupiga kura na kampeni za uchaguzi ambako ilitarajiwa kuwa Rais Kagame ambaye ameiongoza Rwanda kwa miaka 24, ataongoza tena kwa muhula wa nne wa miaka mitano.

Kagame ambaye ni mwanajeshi kitaaluma wakati wa kampeni zake alisema mara kadhaa kwamba angeshinda uchaguzi huo kutokana na mchango wake katika maendeleo ya Rwanda, na kwamba alikubali kugombea ili kukidhi mahitaji ya raia waliomwomba siku zote kugombea tena

Baada ya kukamilisha kampeni za uchaguzi alisema kwamba anaendelea kuwaomba wanachama wa chama chake kuendelea kufikiria mtu atakayechukua nafasi yake hapo baadaye kwani kwa maoni yake wakati umefika mtu mwingine achukue hatamu za uongozi.

Rais Kagame anapongezwa kuinua uchumi wa Rwanda na kuihakikishia nchi hiyo usalama wa kutosha lakini mashirika ya haki za binadamu yamekuwa yakiulaumu utawala wake kushindwa kuwavumilia wapinzani. Madai yanayopingwa vikali na serikali yake wakisema wanaosema hayo ni wale wenye nia mbaya na taifa hilo.

Mwaka 2015 katiba ya Rwanda ilifanyiwa mabadiliko na kumwongezea haki ya kugombea mihula mingine miwili ya miaka mitano, hiyo ikiwa na maana kwamba baada ya muhula huu Kagame ana haki kwa mujibu wa katiba ya Rwanda ya kugombea muhula mwingine.

**VOA**



Moshi ukioneka kufuka baada ya maofisa usalama nchini Kenya kurusha vitoa machozi ili kuwatawanya vijana walioandamana tena katika maeneo mbalimbali nchini humo jana. **PICHA: MTANDAO**

# Maandamano yafanyika tena Kenya

**NAIROBI,** KENYA

MAANDAMANO ya amani yamerejea kote nchini Kenya kudai uwajibikaji na kuwakumbuka waliouawa katika wiki tatu za kupinga muswada wa fedha wa 2024 ambao Rais William Ruto alikataa kuusaini.

Ilielezwa kuwa hali ilikuwa ya wasiwasi katikati ya jiji la Nairobi ambako maduka yalifungwa na idadi ya watu waliokuwa wakitembea ikiwa sio ya kawaida. Huku polisi wakifanya doria na baadhi ya barabara zikiwa zimefungwa.

Wakati maandamano hayo yakiendelea ilielezwa kuwa polisi walifyatua makopo ya gesi ya kutoa machozi ili kuwatawanya waliokuwa wanakusanyika. Licha ya kwamba wengi wao walijihami na maji waliyoyatumia kuosha nyuso zao, na kwamba pikipiki kadhaa zilitelekezwa wakati wa mshike mshike huo.

Polisi waliojihami walionekana nje ya ofisi muhimu za serikali kama Ikulu ya Nairobi, bunge la taifa na mahakama ya juu. Huku dhamira ya maandamano hayo ikitajwa kuwa ni kuishinikiza serikali kuwajibika ukizingatia mauaji ya wanaharakati pamoja na ambao hawajulikani waliko.

Aidha, hadi sasa serikali imekiri kuwa idadi ya waandamanaji waliopoteza maisha yao ni 25, huku takwimu za Shirika la kitaifa la Kutetea Haki za Binadamu (KNCHR), ikielezea mauaji ya watu 41 na majeruhi 360.

Kaimu Inspekta Mkuu wa Polisi, Douglas Kanja, aliwatahadharisha waandamanaji hao kwamba wanapanga kuwavuruga, huku akiwasisitiza kudumisha utulivu na kushirikiana na maofisa wa usalama.

Huko Kisumu, waandamanaji walisema lengo lao ni kuishinikiza serikali kuu kuwajibika na wala sio kuhangaisha uongozi wa serikali ya kaunti.

Yote hayo yakiendelea, Shirika la kutetea Haki za Binadamu la Human Rights Watch linaitolea wito Shirika la Fedha Duniani, (IMF), kufanya kazi kwa pamoja katika utekelezaji wa mpango wake wa kiuchumi na kutimiza haki za binadamu.

Muswada wa fedha wa 2024 ukizingatia mpango huo wa IMF na Kenya, ulitarajia kukusanya dola bilioni 2.7 za Marekani za pato la ziada katika mwaka mpya wa fedha ikiwa ni baadhi ya masharti ya IMF.

**DW**

# Trump amchagua Vance mgombea mwenza

**NEW YORK,** MAREKANI

ALIYEKUWA rais wa zamani wa Marekani, Donald Trump, anayetarajia kushiriki katika kinyang'anyiro cha urais, amemteua seneta wa jimbo la Ohio JD Vance kama makamu wa rais na mgombea mwenza wake.

Hatua hiyo imefikiwa jana baada ya wajumbe wa Chama cha Republican kumchagua rasmi Trump kama mgombea wa urais wa chama hicho katika mkutano mkuu wa chama uliofanyika Milwaukee.

Hayo yanafanyika chini ya siku mbili baada ya Trump kunusurika katika jaribio la kuuliwa katika mkutano wa kampeni huko Pennsylvania.

Ilielezwa kuwa kura ya wajumbe wa Republican kwa Trump inahakikisha kwamba ni wazi sasa rais huyo wa zamani wa Marekani, atakiongoza chama hicho kwa mara ya tatu mfululizo kama mgombea wao katika uchaguzi mkuu.

Pia ilielezwa kuwa mtoto wa Trump, Eric ndiye aliyetangaza matokeo ya kura hiyo ya wajumbe huko Florida, na wimbo wa sherehe ulipigwa huku wajumbe wakionekana wakicheza pamoja na kuonesha mabango yenye picha ya mteule huyo.

Wajumbe wa Republican walionyesha kufurahishwa pia na jaji aliyekuwa anaisikiliza kesi ya nyaraka za siri iliyokuwa inamkabili Trump kuachana na kesi hiyo na kumpa ushindi mkubwa wa kortini mwanasiasa huyo.

Mbali na kumchagua rasmi Trump kama mgombea wa chama hicho, wajumbe kutoka kote nchini Marekani watageukia katika kuweka sera mpya katika jukwaa la sera la chama hicho, jambo hilo likiwa linafanyika kwa mara ya kwanza tangu 2016.

Hatua hiyo inaonesha kwamba timu ya kampeni ya Trump haina nia ya kuwapa Wademocrat mada yoyote ile watakayoitumia katika kampeni yao.

Kwa sasa Wademocrat wamepunguza mipango yao ya kutoa ujumbe wa ushindani wakati wa mkutano huo mkuu wa chama cha Republican na wameyaondoa matangazo yao ya kampeni hasa baada ya jaribio lililolenga Trump.

**DW**

# MASHUJAA YAZIBOMOA BIASHARA, MBEYA CITY

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Mashujaa imeendelea na kampeni yake ya kukiimarisha kikosi chake kwa ajili ya msimu ujao wa Ligi Kuu na mashindano mengine baada ya kusajili wachezaji kutoka Biashara United ambayo ilishindwa kupanda Ligi Kuu msimu huu, ikiishia hatua ya ,play off' na Mbeya City, zote kutoka Championship.

Kwa mujibu wa Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Hussein Bunu, waliosajiliwa ni Mathew Michael kutoka Mbeya City na Carlos Protas kutoka Biashara United.

"Ni wachezaji wazuri, nadhani watatusaidia katika kuimarisha kikosi chetu kuelekea msimu ujao," alisema kocha huyo.

Carlos ambaye ni beki wa kati, ameshawahi kuzichezea Klabu za Toto Africa, Namungo FC, Tusker ya Kenya, kabla ya kutua Biashara United.

Mbali na wachezaji hao, tayari Mashujaa FC imeshawatangaza wachezaji, Ismail Mgunda, kutoka Singida Black Stars, Robert Mathias Makidala na golikipa, Yusuph Dunia, wote kutoka KenGold, na Ally Nassor ,Ufudu', akitokea Kagera Sugar.

Mashujaa ambayo ilicheza Ligi Kuu mara ya kwanza msimu uliopita ilimaliza nafasi ya nane ya msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini ikisubiri mpaka mechi ya mwisho kuweza kuamua hatima yake kwa kuifunga Dodoma Jiji mabao 3-0 na kuinusuru na hatari mbili zilizokuwa zikiikabili, kushuka daraja au kwenda kucheza mechi za mchujo, ,play off.'

**KIROHO SAFI...**



Winga wa Yanga, Farid Mussa (kulia), akimkabidhi jezi namba 17, Kiungo wa timu hiyo. Clautos Chama, aliyejiunga na mabingwa hao wa Ligi Kuu Bara baada ya kumaliza mkataba wake na Simba. Chama akiwa Simba alikuwa akivaa jezi namba 17, hivyo Farid ameridhia kumpa jezi hiyo na yeye sasa atakuwa akivaa uzi namba 12. **PICHA: YANGA**

# FILAMU 70 KUWANIA TUZO TAMASHA LA ZFF

**Na Moshi Lusonzo**

FILAMU 70 kutoka mataifa mbalimbali duniani zimeteuliwa kuwania tuzo katika Tamasha la Kimataifa la Filamu la Zanzibar (ZIFF), litalakaloanza Agosti Mosi, mwaka huu.

Akizungumza katika hafla iliyofanyika katika Kituo cha Utamaduni cha Ujerumani (Gaethe) jijini Dar es Salaam jana, Ofisa Mtendaji wa ZIFF, Joseph Mwale, alisema idadi hiyo inatokana na uchambuzi wa kina uliofanywa kati ya filamu 5,000 zilizotumwa kuomba kuwania tuzo hizo.

Aidha, alisema tamasha hilo litakalofanyika Zanzibar kwa siku nne, vipengele vitakavyoshindaniwa ni, filamu bora ndefu, fupi bora, filamu bora ya Afrika Mashariki na Mwigizaji bora wa kike na kiume Afrika Mashariki.

Pia, vipengele vingine ni mwigizaji bora wa kike na kiume Tanzania, tuzo ya mwenyekiti, mafanikio katika maisha ya filamu na chaguo la watu ambalo litatokana na tamthilia zinazorushwa katika televisheni katika nchi za Afrika Mashariki.

"Kwa mara ya kwanza ZIFF itakuwa na siku maalum ya kitaifa Julai 31, mwaka huu, ikiwa ni sehemu ya kukaribisha ufunguzi wa tamasha kwa kuonyesha filamu ya aina yake inayoelezea nyumba ya maajabu maarufu Kisiwani Zanzibar," alisema Mwale.

Mwale alisema licha ya maonyesho ya filamu, pia kutakuwa na warsha mbalimbali zitakazotoa elimu kuhusu uigizaji, usimamizi na utengenezaji filamu na mashindano ya ngalawa.

Balozi wa Umoja wa Ulaya nchini, Christine Grau, alisema anajivunia kuona tamasha hilo linazidi kuwa na nguvu na alama ya kitamaduni duniani.

Alisema umoja huo utaendelea kufadhili ZIFF kila mwaka kwa sababu uwapo wake unaongeza mwanga, juhudi na ukuzaji vipaji kwa jamii ya Kitanzania na Afrika kwa ujumla.

# Taifa Ufukweni waifuata Zanzibar

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Tanzania ya Soka la Ufukweni, inatarajiwa kuondoka Ijumaa ya wiki hii kuelekea Zanzibar kwa ajili ya kucheza michezo miwili ya kirafiki dhidi ya Timu ya Taifa visiwani humo.

Akizungumza na Nipashe, Kaimu Kocha Mkuu wa timu hiyo, Raruph Rajab, alisema wameamua kwenda kucheza na timu hiyo kutokana na kutambua ubora wake.

„Ijumaa tutaondoka kwenda visiwani Zanzibar kwa ajili ya kucheza michezo hiyo ikiwa ni mwendelezo wa maandalizi ya michuano ya AFCON kwa timu za ufukweni, itakayochezwa Agosti 26-30 nchini Misrit," alisema Rajab.

Alisema leo jioni watacheza mchezo wa kirafiki na timu ya Kombaini ya Soka la Ufukweni inayoshiriki Ligi Kuu mchezo ambao utapigwa majira ya saa 9:00 alasiri.

# KenGold haitanii, yajichimbia Tukuyu

**Na Adam Fungamwango**

KIKOSI cha KenGold kilichopanda daraja na kutarajia kucheza Ligi Kuu kwa mara ya kwanza msimu unaokuja, kimeamua kujichimbia Tukuyu, Rungwe mkoani Mbeya kwa ajili ya maandalizi ya msimu mpya wa mashindano.

Katibu Mkuu wa timu hiyo, Benson Mkocha, alisema wameamua kutimkia huko kutokana na hali ya hewa kuwa nzuri na rafiki kwa wachezaji, lakini kukwepa mwingiliano wa watu wengi, ikiwamo mashabiki.

"Tumeondoka nyumbani Chunya, tumekwenda kupiga kambi Tukuyu, tumeondoa timu kwa sababu huko hali ya hewa ni nzuri zaidi kwa wachezaji kupokea mazoezi, hasa kipindi hiki ambacho wanatakiwa kufanya magumu na kwa muda mrefu kwa ajili ya kujenga stamina na pumzi.

Lakini pia tunahitaji utulivu, wachezaji kwa sasa hawahitaji mwingiliano wa watu wengi, badala yake wanatakiwa wakifanya mazoezi wapumzike, wamsikilize kocha, unajua wakati mwingine mazoezi yakifanywa kukiwa na mashabiki, mchezaji badala ya kufanya kile ambacho mwalimu anafundisha yeye anataka kufurahisha mashabiki," alisema Katibu Mkuu huyo.

## ZISIKUPITE

### HOWE ATAJWA ENGLAND

KOCHA wa Newcastle United, Eddie Howe ni mmoja wa makocha wanaopigiwa upatu kuchukua nafasi ya Gareth Southgate, iwapo ataamua kujiuzulu kama kocha wa Timu ya Taifa ya England. Wachezaji wa zamani wa England, Steven Gerrard na Frank Lampard pia wanatazamiwa kuwania nafasi hiyo. ***(Guardian)***

### TAH AULIZIWA UNITED

KLABU ya Manchester United imemuulizia beki wa Ujerumani, Jonathan Tah, huku Bayern Munich wakishindwa kufikia makubaliano na Bayer Leverkusen kumsajili mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28. ***(Florian Plettenberg)***

### ARSENAL YAMZUIA ROWE

KLABU ya Arsenal imekataa ofa ya Fulham ya kutaka kumnunua kiungo wa kati wa England, Emile Smith Rowe, 23. ***(Standard)***

### LIVER, ATLETICO ZAVUTANA

LIVERPOOL na Atletico Madrid zinavutiwa na mlinzi wa RB Leipzig, Mfaransa Mohamed Simakan, 24. ***(Sky Germany)***

### MORATA KUTUA MILAN

MSHAMBULIAJI wa Hispania, Alvaro Morata mwenye umri wa miaka 31, anatazamiwa kujiunga na AC Milan kwa mkataba wa miaka minne kutoka Atletico Madrid. ***(Fabrizio Romano)***

### MERINO ALENGWA BARCA

NYOTA wa Hispania, Mikel Merino ni mmoja wa wachezaji wanaolengwa na Barcelona kuimarisha safu yao ya kati, huku mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 akiwa amesalia na mwaka mmoja kwenye mkataba wake na Real Sociedad. ***(Mundo Deportivo)***

### ARSENAL NAO WAJITOSA

ARSENAL pia wanapania kumnunua Mikel Merino, ambaye aliwahi kuichezea Newcastle United kabla ya kurejea Hispania. ***(Telegraph)***

### AUBAMEYANG ATAJWA SAUDIA

MSHAMBULIAJI wa Gabon, Pierre-Emerick Aubameyang mwenye umri wa miaka 35, anakaribia kujiunga na Klabu ya Saudi Arabia ya Al-Qadsiah. ***(Sky Sports)***

### OLMO HUYOOO CITY

KLABU ya Manchester City imepiga hatua katika juhudi za kumsajili kiungo wa kati wa Hispania, Dani Olmo mwenye umri wa miaka 26, kutoka RB Leipzig. ***(Football Insider)***


### BAYERN, CITY MBIO MOJA

KLABU ya Bayern Munich pia inavutiwa na Dani Olmo anayewindwa na Manchester City, ambaye alifunga mabao matatu wakati wa Euro 2024 alipoisaidia nchi yake ya Hispania kushinda michuano hiyo. ***(Fabrizio Romano)***

### GNONTO NA NEWCASTLE

KLABU ya Newcastle United iko tayari kumenyana na Everton katika harakati za kumsajili winga wa Italia, Wilfried Gnonto mwenye umri wa miaka 20 kutoka Klabu ya Leeds United. ***(Teamtalk)***

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# GIROUD ASTAAFU UFARANSA

**●●●Aiachia mabao 57 huku akielekea kukipiga Marekani baada ya kusaini...**

**PARIS,** UFARANSA

MFUNGAJI bora wa muda wote wa Ufaransa, Olivier Giroud, alithibitisha kumalizika kwa soka lake la kimataifa Jumatatu, akiwa tayari kuanza kucheza na klabu yake mpya ya LAFC katika Ligi Kuu ya Marekani, MLS.

Giroud alisema kabla ya michuano hiyo kwamba ataichezea Ufaransa kwa mara ya mwisho kwenye mashindano ya Ulaya.

"Wakati ambao nimekuwa nikiuogopa umefika. Wakati wa kuaga Timu ya Ufaransa," alisema Giroud mwenye umri wa miaka 37, akiandika kwenye ukurasa wake wa Instagram siku ya Jumatatu.

Ufaransa ilipoteza kwa mabao 2-1 kutoka kwa Hispania katika fainali ya Euro. Giroud alikuwa mchezaji wa akiba kipindi cha pili katika mchezo wake wa mwisho kwa Ufaransa.

Alifunga mabao 57 katika mechi 137 za Ufaransa na alikuwa mshiriki wa kikosi kilichoshinda Kombe la Dunia la mwaka 2018.

Giroud ataendelea na uchezaji katika Ligi ya MLS baada ya kusaini kuicheza LAFC, akiondoka Ulaya baada ya miaka 18 katika Ligi Kuu za kulipwa nchini Ufaransa, England na Italia.

Alijiunga na LAFC akitokea AC Milan kwa mkataba hadi 2025 ambao una kipengele cha kuongeza mwaka mmoja hadi 2026.

Mshambuliaji huyo anafahamika zaidi kwa misimu sita aliyoichezea Arsenal kuanzia 2012-18, akifuatiwa na Chelsea na Milan kwa miaka mitatu kila moja.

Ana mabao 285 katika mechi 716 za klabu na mataji yake ni pamoja na Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2021 akiwa na Chelsea.

Pia alishinda Ligi ya Ufaransa akiwa na Montpellier mnamo 2012, na Serie A akiwa na Milan miaka 10 baadaye.

# ARAUJO NJE YA DIMBA MIEZI MINNE

**BARCELONA,** HISPANIA

MLINZI wa Barcelona, Ronald Araujo, anatazamiwa kuwa nje ya uwanja kwa takriban miezi minne baada ya kuamua kufanyiwa upasuaji wa tatizo la misuli ya paja, vyanzo vilithibitisha kwa ESPN.

Araujo mwenye umri wa miaka 25, alijeruhiwa katika ushindi wa robo fainali kati ya Uruguay na Brazil kwenye Copa America na akakosa mechi zilizosalia.


Baada ya kushauriana na timu ya madaktari wa Barca, sasa ameamua kufanyiwa upasuaji kwenye misuli ya paja iliyojeruhiwa.

Klabu hiyo ya Katalunya haijaeleza ni muda gani atakuwa nje ya uwanja, lakini vyanzo viliiambia ESPN kuwa hakuna uwezekano wa kurejea Novemba mwaka huu.

"Vipimo vimeonesha kuwa Araujo ana jeraha la msuli wa kulia," ilisema taarifa ya Barca.

"Atafanyiwa upasuaji unaoongozwa na Dk. Lasse Lempainen, akisimamiwa na wahudumu wa afya wa klabu hiyo, nchini Finland. Baada ya utaratibu huo, taarifa ya matibabu itatolewa."

Barca ilirejea kwenye mechi za kujiandaa na msimu mpya wiki iliyopita chini ya kocha mpya, Hansi Flick na wataanza kampeni ya LaLiga ya 2024-25 dhidi ya Valencia Agosti 17.




# Lazio wapambana kumsajili Greenwood

**ROME,** ITALIA

RAIS wa Lazio, Claudio Lotito, amedai Juventus na Napoli zote zinajaribu kuteka mpango wake wa kumnunua mshambuliaji wa Manchester United, Mason Greenwood.

United wamemfahamisha Greenwood, ambaye aliona mashtaka ya kujaribu kubaka, kushambulia na kudhibiti nguvu yakitupiliwa mbali kabla ya mkopo wa muda mrefu kwa Getafe, kwamba hana mustakabali wa kuishi Old Trafford na wako kwenye mazungumzo na klabu kadhaa juu ya kuuzwa msimu huu wa majira ya joto.

Miamba wa Ufaransa Marseille wanaripotiwa kufikia makubaliano ya kumsaini Greenwood, ingawa meya wa jiji hilo ameitaka klabu hiyo kutoendelea na uhamisho huo kwa sababu ya historia ya madai dhidi ya fowadi huyo.



Lazio wana matumaini ya kushinda katika kinyang'anyiro cha kuwania saini ya Greenwood, lakini Lotito aliiambia Il Messaggero kwamba kuna klabu kadhaa pia zinajaribu kumwania.

"Nilitoa ofa ya euro milioni 25 pamoja na asilimia 50 ya mauzo, pamoja na bonasi na kamisheni," Lotito alifichua.

"Na bado kuna klabu kadhaa zimeingia kufanya fujo. Juventus, Napoli ... inaonekana kwamba kila mtu anapiga kelele. Wanaogopa tunaweza kumchukua na wanataka kuharibu kila kitu.

"Ndiyo, nilisema kuna shabaha nyingine ambaye ana nguvu mara kumi zaidi ya Greenwood. Ni kweli, lakini nina jina lingine changa lililofichwa."

Marseille inafahamika kuwa wamefikia makubaliano yenye thamani ya pauni milioni 27.6 pamoja na bonasi, na bado haijabainika kama bonasi za Lazio zitalingana na ada ya ofa kutoka kwa timu hiyo ya Ufaransa.

Greenwood amezungumza na maofisa wa United katika uwanja wa mazoezi wa klabu hiyo wa Carrington msimu huu wa majira joto ili kuthibitisha kwamba mustakabali wake uko mbali na klabu hiyo.

# Kane: Nina sononeka moyoni

**LONDON,** ENGLAND

NAHODHA wa England, Harry Kane, amesema „nimeumia moyoni" wakati timu hiyo ikirejea England kutoka Ujerumani baada ya kufungwa mabao 2-1 na Hispania kwenye fainali ya Euro 2024.

England ilipokea kichapo hicho huku mchezaji wa akiba Mikel Oyarzabal akifunga bao la ushindi dakika za lala salama mjini Berlin Jumapili.

Nico Williams alifunga bao la kwanza katika ushindi wa Hispania dakika mbili za kipindi cha pili, na licha ya bao la kusawazisha la Cole Palmer, La Roja ilimaliza kwa ushindi - na kutwaa taji lao la nne la ubingwa wa Ulaya.

Kane aliandika kwenye ukurasa wake wa X: „Tumevunjika moyo hatukuweza kufikia kile tulichofanyia kazi kwa bidii. Ilikuwa ni michuano migumu ya muda mrefu na ninajivunia vijana na wafanyakazi kufika fainali.

"Mwishowe tulishindwa kufikia lengo letu na tutalazimika kuishi na hilo, lakini kama tunavyofanya siku zote tutajiinua, kujivua vumbi na kuwa tayari kupigana tena tukiwa na jezi ya England.

"Asante kwa mashabiki wote waliotuamini na kutuunga mkono hadi mwisho!"

Kocha Gareth Southgate na wachezaji wa England walishangiliwa na mashabiki walipokuwa wakiondoka kwenye hoteli yao mjini Berlin.






# Aucho ampasua kichwa Andambwile

INATOKA UK. 24

sana kujiunga na timu kama Yanga ambayo kwa sasa ina mafanikio makubwa na wachezaji wakubwa, huku yeye mwenyewe akitarajiwa kuwa atakuwa mmoja wa watu wenye mafanikio ya hao aliowakuta.

"Kila mmoja ana ndoto kucheza timu yenye mafanikio makubwa kama Yanga, na mimi pia baadaye nitakuwa ni mmoja kati wachezaji wenye mafanikio kwa mataji," alisema mchezaji huyo ambaye kabla ya kujiunga na kikosi cha Fountain Gate, aliichezea Mbeya City.

Alionyesha furaha yake alipowakuta wachezaji wenzake ambao amezoeana nao kabla hata ya kujiunga na kikosi hicho.

"Nimekutana na rafiki zangu hapa, Kibwana Shomari na Dickson Job tunafahamiana kabla sijafika na wao ndiyo wanaonifanya niwe kama mzoefu hapa, nimefurahi sana," alisema.

Aliwaahidi wanachama na mashabiki wa Yanga kuwa watamuona Andambwile yule yule waliokuwa wakimuona akiwa Mbeya City na baadaye Singida Fountain Gate.

Hata hivyo kiungo huyo atakuwa na changamoto kubwa kwani atakutana na Khalid Aucho, mmoja wa viungo wakabaji bora nchini, na Mudathir Yahaya, ambaye mbali na kukaba, lakini ana uwezo mkubwa wa kupachika mabao.

# AZAM: HATUIOGOPI PYRAMIDS

**Adam Fungamwango na Shufaa Lyimo**

KLABU ya Azam FC imesema licha ya Pyramids ya Misri kuonekana kama kikwazo kwenye njia yao ya mafanikio ya michuano ya kimataifa, lakini malengo yao bado yapo pale pale ya kutinga hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Mwenyekiti wa klabu hiyo, Nassor Idrissa ,Father', amesema jana kuwa msimu huu wamejipanga kufanya vema na kwamba haijalishi ni mpinzani gani aliyekuwa mbele yao.

Azam imepangwa kucheza dhidi ya APR ya Rwanda katika mechi ya raundi ya awali, Ligi ya Mabingwa Afrika, ikianzia nyumbani Agosti 16 hadi 18, kabla ya marudiano, Agosti 23 hadi 25, mwaka huu, na baada ya hapo itacheza na mshindi kati ya JKU ya Zanzibar dhidi ya Pyramids katika michezo ya raundi ya kwanza inayotarajiwa kuchezwa Septemba 13 na marudiano yake yatakuwa Septemba 20, mwaka huu.

"Kihistoria hii ni mara yetu ya pili kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika, tuliwahi kucheza huko nyuma na tuliondolewa na El Merrikh ya Sudan, hii tunarudi kwa mara ya pili sasa, lengo letu ni kucheza hatua ya makundi, tukifika hatua hiyo sisi kama klabu tutakuwa hatuna deni kabisa, ila siyo kwamba tukifika tutasema imetoka tunajitoa, hapana, tutapambana ili kwenda mbele zaidi na tutakuwa tumekwenda juu ya malengo yetu.

"Tunaomba tu vijana wetu wasipate matatizo ya kiafya ili tutimize malengo yetu na tunamatumaini makubwa sana ya kufanya vema msimu huu na haijalishi wapinzani waliokuwa mbele yetu," alisema Father.

Alisema pamoja na kwamba watu wanaizungumzia zaidi mechi yao dhidi ya Pyramids ambayo haijafika, lakini wao wanaiangalia APR kama ndiyo kikwazo chao, kwani wanatakiwa kwanza waitoe mashindanoni ndiyo waanze kuipigia mahesabu mechi inayofuata.

"Ni kweli hatuna rekodi nzuri kwenye michuano ya kimataifa, ni kweli watu wanaiangalia zaidi Pyramids, lakini mbele yetu kwanza yupo APR, lazima kwanza tuwatoe ndiyo tufike huko, hatutaki kumfikiria mpinzani anayefuata kabla ya kucheza naye, haya mambo yalishatugharimu sana huko nyuma, kwa hiyo kwanza tumtoa yeye ndiyo twende huko kwa Pyramids, naye naamini tutamuondoa," alisema.

Mara ya mwisho kwa Azam kucheza Ligi ya Mabingwa Afrika ilikuwa ni 2015, iliposhinda mabao 2-0 dhidi ya El Merrikh mechi ya raundi ya kwanza, Februari 15, lakini ikashindwa kutinga hatua ya makundi, ilipochapwa mabao 3-0, Februari 28, katika mechi ya marudiano.

Wakati huo huo Kocha Mkuu wa Azam FC, Youssouph Dabo, amesema kambi waliyoiweka nchini Morocco itawasaidia kujiandaa vizuri ili kutoa ushindani kwenye mchezo wao wa Ngao ya Jamii, Ligi Kuu pamoja na ile ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Akizungumza na Nipashe moja kwa moja kutoka nchini humo, alisema wanaendelea vema na mazoezi na kudai kila mchezaji ana morali ya juu.

"Huku tunaendelea vizuri kila mchezaji ana ari ya juu kuelekea msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara utakaoanza mwezi ujao," alisema Dabo.

Hata hivyo alisema miongoni mwa vitu atakavyovifanya katika kambi hiyo ni kucheza michezo mingi ya kirafiki ambayo itawasaidia wachezaji wake kuwa imara zaidi.

Aliongeza kuwa malengo yake ni kutwaa ubingwa msimu ujao na kuwataka mashabiki wao waendelee kuwapa ushirikiano ili watimize malengo yao.

# Sakata la Lawi Simba, Coastal mtihani kwa TFF

INATOKA UK. 24

"Tunaimani na hivi vyombo vinavyosimamia, maamuzi yakiamua mchezaji aende Simba bure bila Coastal Union kupata chochote tutaridhia, pia tukiambiwa Lawi abaki basi hatuna pingamizi, tunaimani na kamati," alisema Katibu huyo.

Kwa upande wa Simba, wanasheria wao baada ya kumalizika kutoa ushahidi wao waliondoka huku kamati ikiendelea kusikiliza mashauri mengine yaliyofika mezani kwao.

Wakati huo huo, winga mpya wa Simba, Joshua Mutale, amebainisha kuwa wachezaji wengi Afrika wanatamani kuichezea klabu hiyo kutokana na kuwa moja ya klabu kubwa barani humo, huku ikiwa ndani ya nafasi kumi kwa ubora.

Akizungumza nchini Ismailia ambako timu hiyo imeweka kambi ya maandalizi ya msimu mpya, Mutale ambaye amesajiliwa msimu huu akitokea Power Dynamos ya Zambia, amesema hata nchini kwao, hakuna mchezaji ambaye akitakiwa na klabu hiyo atakataa, kwani imejipambanua kwa kuwa na ubora chini ya Jangwa la Sahara, ukiondoa Mamelodi Sundowns na TP Mazembe.

"Nimekuja Simba ili irudie kutwaa mataji, kama ni ubora imeshakuwa bora barani Afrika na kila mchezaji barani humu anapenda kuichezea klabu hii, nami pia nimefurahi kupata bahati hiyo, lakini hiyo haitoshi, ni lazima mtu ufanye kazi ya ziada ili ukubalike na mashabiki ambao nguvu yao nimeiona hata kwenye mitandao ya kijamii, lakini kuipatia mafanikio klabu," alisema.

Alisema hasemi kwa sababu amejiunga na timu hiyo, ila viwango vya ubora kutoka Shirikisho la Mpira wa Miguu Afrika (CAF), ndivyo vinaongea, kuwa ni moja kati ya timu tatu ambazo zipo kwenye kumi bora ya viwango vya Afrika chini ya ukanda huo, huku saba zilizobaki zinatoka Afrika Kaskazini.

"Kwa ubora huu, sidhani kama kuna mchezaji yeyote anaweza kuikataa nafasi hii, ndiyo maana walivyokuja tu kuniambia wananihitaji, sikutaka tena kuongeza mkataba kwenye timu yangu," alisema.

Alisema kingine kilichomfanya akubali kutua Simba ni rekodi nzuri ya wachezaji wa Kizambia waliopita kwenye klabu hiyo.

"Wachezaji wengi wa Zambia waliopita hapa wamefanya vizuri kama Felix Sunzu, Clatous Chama na Moses Phiri, rekodi hii imenivutia sana, naamini hata mimi nitafuata nyayo zao na nafikiri ndiyo maana klabu hii imekuwa ikiwaamini wa kutoka kwetu," alisema.

# Prisons yamnasa straika wa Dodoma Jiji

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Prisons, imefanikiwa kupata saini ya straika Meshack Abraham Mwamita, akitokea Dodoma Jiji, huku ikipandisha wachezaji saba kutoka kikosi cha vijana cha timu hiyo chini ya miaka 20.

Taarifa iliyotolewa jana na Idara ya Habari na Mawasiliano ya klabu hiyo, imesema usajili huo umefanyika ili kuboresha safu yao ya ushambuliaji, ambapo wana imani kuwa Mwamita atakwenda kutibu tatizo hilo.

"Tumemsajili Mwamita na tunamkaribisha katika familia ya Wanajelajela," ilimaliza taarifa ya klabu hiyo yenye maskani yake jijini Mbeya.

Kabla ya kujiunga na Prisons, straika huyo alikuwa akiichezea Dodoma Jiji msimu uliopita, ambapo alianza kuchezaji Ligi Kuu kwa mara ya kwanza 2021, akiwa na Klabu ya Gwambina, na iliposhuka daraja alihamia Kagera Sugar, hadi 2023, alipotua Dodoma.

Kabla ya kuinasa saini ya mchezaji huyo, Prisons ilitangaza kuwanasa wachezaji, winga Haruna Chanongo kutoka Pamba FC, straika Oscar Mwajanga kutoka Mbeya Kwanza, na golikipa Sebusebu Samson kutoka Geita Gold.

Klabu hiyo inayomilikiwa na Jeshi la Magereza, imetangaza kupandisha wachezaji saba wanaotoka kwenye kikosi cha vijana chini ya miaka 20.


Imesema kwa sasa wachezaji hao wameshaungana na kikosi cha wakubwa tayari kwa maandalizi ya msimu ujao wa mashindano chini ya Kocha Mkuu, Mbwana Makata.

Wachezaji hao ni, Kelvin Sengati, Ashraf Mbonde, Erick Mwampenja, Yohana Mgella, Joah Mwakilema, Ally Hamza na Evance Dalf.

Michezo
Nipashe Jumatano Julai 17, 2024

## Giroud astaafu Ufaransa

UKURASA 21



●●● Kamati sasa kuamua, Mutale naye asema nyota wengi Afrika wanatamani kuichezea...

HAPA KAZI TU...



Winga wa Simba, Edwin Balua (jezi nyekundu), akipata upinzani mkali kutoka kwa beki wa kati wa timu hiyo, Che Malone, wakati wakiwa kwenye mechi ya mazoezi kambini Ismailia nchini Misri jana. **PICHA: SIMBA**

# Sakata la Lawi Simba, Coastal mtihani kwa TFF

**Na Waandishi Wetu**

SAKATA la klabu ipi ina haki ya kummiliki beki Lameck Lawi, kati ya Simba na Coastal Union bado limebaki mikononi mwa Kamati ya Hadhi na Haki za Wachezaji iliyopo chini ya Shirikisho la Soka nchini (TFF), baada ya pande mbili jana kutoa maelezo mbele ya kamati hiyo, imeelezwa.

Lawi msimu uliomalizika aliichezea Coastal Union na ulipomalizika akauzwa Klabu ya Simba, lakini wamiliki wake hao wa zamani walirejesha hela kwa madai muda waliowekeana wa malipo ulimalizika, jambo ambalo limezua mvutano kwani upande wa pili pia unasema ulifuata taratibu zote.

Hata hivyo, jana kila upande ulitoa ushahidi wake mbele ya kamati hiyo, Coastal Union, ikiwakilishwa na Katibu Mkuu wake, Omary Ayoub, huku Simba ikiwakilishwa na wanasheria wao.

Akizungumza na Nipashe baada ya kutoa ushahidi mbele ya kamati hiyo Makao Makuu ya TFF, Karume, Ilala jijini Dar es Salaam jana, Katibu wa Coastal Union, Ayoub alisema shauri la beki wao, Lawi bado lipo chini ya Kamati ya Hadhi na Haki za Wachezaji sasa ndio watakaoamua endapo ni mchezaji wa Simba au atabaki Coastal Union.

Ayub alisema kuwa waliitwa kwenye kamati na kusikilizwa pande zote mbili na sasa wanasubiri shauri na maamuzi kutoka kwenye kamati hiyo.

INAENDELEA UK. 23

# Aucho ampasua kichwa Andambwile

**Na Adam Fungamwango**

KIUNGO mkabaji mpya wa Yanga, Aziz Andambwile, amesema ilikuwa ni ndoto yake kujiunga na klabu hiyo, hivyo kitu kikubwa zaidi kwake ni kupambana ili kupata namba katika timu hiyo yenye wachezaji wakubwa na mahiri Afrika.

Akizungumza akiwa kambini Kigamboni, Dar es Salaam, alisema hata baba yake mzazi baada ya kusikia habari za kusajiliwa Jangwani alimuusia kuwa ajichunge na kwenda kupambania namba na si kitu kingine.

Andambwile, mmoja wa viungo wakabaji wanaokuja juu kwa sasa nchini, amesajiliwa hivi karibuni na Yanga, akitokea Singida Fountain Gate.

"Nimepata mapokezi makubwa kutoka kwa wenzangu, safari yangu ya soka ni ndefu sana hadi hapa nilipofika na kwa sababu nimepata nafasi hii adimu ya kufika Yanga, inabidi nipambane ili kuipata namba, kwa hiyo niko tayari kwa hilo, hata baba yangu mzee Andabwile baada ya kusikia nimesaini Jangwani, alinipa nasaha zake, akaniambia unakwenda kukutana na watu wapya, changamoto mpya, hivyo kazi kubwa ni kujichunga na kupambania nafasi mwanangu," alisema.

Alisema kuwa anajisikia furaha

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >